# TOENI FATWA

Na

**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian**

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

Toeni Fatwa

*Istiftā'* (Kiurdu)

(Swahili Translation)

Mwandishi:

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

Mfasiri: Sheikh Bakri Abedi Kaluta

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1897

Chapa ya Kwanza (Kiswahili): Tanzania 2016

Kwa maelezo zaidi:

Tanzania:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania

Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.

Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:

E.A. Ahmadiyya Muslim Mission

P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +255222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press

Dar es Salam, Tanzania

Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-548-4

# Maelezo Ya Mwenezi

Twamshukuru Mwenyezi Mungu Aliyetujalia kufululiza kuwaletea wasomaji wa Kiswahili hazina za kiroho zenye thamani kubwa sana.

Kisa chenyewe ni kuwa kiongozi mmoja wa dhehebu la Aria, jina lake Lekhram, alizoea kutumia midomo michafu sana dhidi ya Mtume[saw] na Islam. Yeye akang'ang'ania kwamba kama dini ya Kiislamu ni kweli, basi Seyidna Ahmad[as] afanye utabiri wowote kwa kuambiwa na Mwenyezi Mungu kumhusu Lekhram, na utabiri huo utimie barabara katika muda wake maalum. Hapo Seyidna Ahmad[as] akatabiri ya kuwa Lekhram atakufa katika muda wa miaka sita kwa kuuliwa. Utabiri huu ukatimia sawasawa, na Lekhram akauawa. Lakini, sasa, wafuasi wake wakaanza kusema kuwa hiyo ilikuwa ni njama tu ya Seyidna Ahmad[as]. Ili kuondolea mbali shutuma hii ya Waaria, Seyidna Ahmad[as] akaandika kitabu cha Istiftaa ambamo akawataka wenye elimu watoe fatuwa baada ya kusoma kwa makini kitabu hicho kwamba je kweli utabiri umetimia au la.

Kitabu hiki kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta. Kisha Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Mbashiri Mkuu wa zamani wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, na Sheikh Adnan Ahmad

Hashimi wa Kenya wakaidurusu tafsiri hii. Mwishowe nikaisoma kwa makini ili kuisogeza karibu zaidi na matini ya Kiurdu.

Sheikh Ansar Hussain na Sayid Tanwir Mujtaba nao wakasaidia kwa njia mbalimbali ili kukamilisha kazi hii kubwa.

Ndugu hao wote wanastahili kushukuriwa. Mwenyezi Mungu Awajalie malipo bora. Amin. Hili ni zao jingine la Dawati la Kiswahili.

Jamil R. Rafiq

Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid

Rabwah, Pakistan

24 Mei 2016

ٹائٹیل طبع اوّل

# اِستفتاء

لَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ

وَمَنْ يَّكْتُمْهَا فَاِنَّهٗٓ اٰثِمٌ قَلْبُهٗ وَاللّٰهُ بِمَا

تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ ۝

گواہی کو مت چھپاؤ۔ اور جو شخص گواہی کو چھپائے اُس کا دِل گنہ گار ہے

اور خدا جو کام تم کرتے ہو جانتا ہے

مطبعِ ضیاء الاسلام قادیان دار الامان میں چھپا

۱۶ - مئی ۱۸۹۷ء

Jalada la mara ya kwanza

# Istiftaa

وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ۚ وَمَنْ يَّكْتُمْهَا فَإِنَّهٗٓ اٰثِمٌ قَلْبُهٗ ۚ وَاللّٰهُ بِمَا
تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ

Msifiche ushahidi, na yule aufichaye ushahidi moyo wake ni wenye dhambi na Mwenyezi Mungu Anayajua myafanyayo.

Kimechapwa katika kiwanda cha uchapaji Dhiaul Islam, Qadian, Darul-Amaan

16 Mei 1897

You should not conceal your testimony, and he who does conseal is surely wicked minded; and God is perfectly aware of what you do. -(Sura Baqar R. 38)

---

Sir,

I beg to enclose herewith a copy of the pamphlet named "Istifta". The motive which has led me write it is, that the Aryas entertain quite a false notion that Lekh Ram was murdered at my instigation. I am inclined to excuse them for this, as they are entirely ingorant of the supernatural origin of prophecies, and according to their belief inspiration and revelation from God belonged only to the hoary antiquity, now they have become extinct, in other words the divine influence is not eternal, but a thing of the past. Therefore they cannot reconcile the prophetic phenomena with the present age. However a study of the pamphlet, it is hoped, will not only clear me of any participation direct or indirect in Lekh Ram's murder, but will also be useful to those who deny the existance of prophetic revelation in this age, and who consider the power of telling future events inconsistent with the laws of Nature. At any rate this pamphlet will probably be interesting and instructive to those who sicncerely seek a reply to the questions:-(1) "Is there a God at all"? (2) "If so, does He reveal future events to His Elite."? I have answere these questions by fully explaining such reasons as conclusively prove that tha prophecy about the Lekh Ram was actually revealed by God, and that it was altogether out of the Province of man's capabilities and device.

I have repeatedly said that Lekh Ram had challenged me to make the prophecy concerning himself which if it were fulfilled was to be the sole criterion of the truth or falsehood of Islam and the Arya faith. And when the prophecy was made, both the parties agreed to give it a very wide publication and awaited the result most anxiously. At last is has been most clearly and definitely fulfilled. The most curious phase of the prophecy, which has been very thoroughly discussed in these pages, is, that it was published in clear and unequivocal words in the"BURAHIN-I-AHMADIYYAH" about seventeen years ago when Lekh Ram was a mere boy of twelve or

☆Istifta is an Arabic word and means to cosult a learned man for an opinion

thirteen years. The readers of this pamphlet, must carefully consider this fact which, I believe, will improve their faculty of discernment, and by cleary shewing them the difference between Divine and human powers, will settle their thoughts and satisfy their minds.

It would not be out of place to invite your attention to another of my books-"SIRAJ-I-MUNIR" or "THE BRIGHT SUN,"- which deals with this important question from another point of view. All the prophecies which were made and literally fulfilled before Lekh Ram's death, have been collected therein, and a few of them concerned some other Aryas who are still alive to bear testimony to what they experienced in their own cases. If any of my readers before attemting a reply to this pamphlet should like to see the "SIRAJ-I-MUNIR" it shall be sent to him with great pleasure.

I should also mention that those Maulvies, who like the Aryas, bewildered by the too accurate and unexpected fulfilment of the prophecy, and who being utterly devoid of spirtuality are befogged by doubt, will find it worth their while to persue this book.

I send this pamphlet to you so that after a careful consideration of the arguments I have given, you may give your impartial opinion as to the following points:-

1. Has the prophecy about Lekh Ram been acutally fulfilled?

2. If so can it be said that the prophecy is suprernatural, that is, neither a design of man nor a mere accident, but a special manifestaion of the Divine powers, which may be termed a revealed prophecy?

And communicate the same with your arguments in support of your views to

Your ever faithful,

Kadian: MIRZA GHULAM AHMED

Dated 1st May 1897 Chief of Kadian,

Gurdaspur District

Punjab.

Imechapishwa katika mtambo wa uchapishaji Dhiaul-Islam Qadian Darul-Amani

وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ۚ وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ

Tafsiri

Wala msifiche ushahidi; na atakayeuficha, basi moyo wake ni wenye dhambi. Na Allah Huyajua mnayoyatenda.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ *

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّیْ عَلٰی رَسُوْلِهِ الْكَرِیْمِ **

Ndugu Mheshimiwa, Pamoja na barua hii nakutumia kijitabu kimoja kiitwacho Istiftaa. Haja ya kuandika kijitabu hiki ilikuwa ni kwamba Waaria wamelisisitiza mno jambo hili kwamba Lekhram aliuawa kutokana na njama zangu. Kwa rai yangu wao, kwa kiasi fulani, wanao udhuru pia, kwa sababu hawanayo habari kabisa ya njia zisizo za kawaida za bishara za kiufunuo. Sababu ni hii kwamba kutokana na itikadi yao ufunuo wa Mungu umekoma tangu maelfu ya miaka, na Neno la Mungu haliko mbele bali limebaki nyuma. Kwa hiyo, wao hawawezi kufahamu kwa njia yoyote ile kwamba kunaweza kutolewa bishara kama hizo pia toka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa vyovyote vile kuzieleza zile sababu tulizonazo za kujiondolea tuhuma sio tu kwa kuziondoa shaka za wapambe wa Lekhram, bali pia kwa kupanua elimu za watu ambao katika zama hizi huipinga maana yenyewe ya utabiri wa kiufunuo na wanafikiria kuyaeleza mambo ya ghaibu kabla ya wakati wake

* Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

** Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

kuwa kinyume na kanuni ya asili. Aghalabu kijitabu hiki kitawavutia na kuwaongezea elimu wale pia ambao kwa shauku ya moyo wanafanya utafiti wa jambo hili kwamba je kweli Mwenyezi Mungu Yupo? Na je Anaweza kumdhihirishia yeyote habari za ghaibu kabla hazijatimia? Kwa kusudio hili hili ndani ya kijitabu hiki mmeelezwa sababu zote zile ambazo zinathibitisha vizuri kabisa kwamba ile bishara iliyotolewa kuhusiana na Lekhram ilikuwa kweli imetoka kwa Mwenyezi Mungu na haiwezekani kabisa kwamba iwe njama ya mwanadamu, au mwanadamu awe na uwezo juu yake. Na mara nyingi tumeshaeleza kwamba ni Lekhram mwenyewe ndiye aliyeomba itolewe bishara hii na akaichukulia kuwa ni kipimo cha kupimia ukweli na uwongo wa Islam na dini ya Kiaria. Na halafu baada ya hayo, kwa maridhiano ya pande mbili, pande zote mbili zikaitangaza sana bishara hiyo na kama vile kunavyokuwepo na mapambano ya washindani mwereka, ndivyo hivyo pande zote mbili zilivyokuwa zikitazama bishara hii. Hatimaye ikatimia kwa uwazi kabisa. Ndani ya bishara hii kuna jambo la ajabu kabisa ambalo nimelieleza ndani ya kijitabu hiki kwa hoja zilizo madhubuti kabisa, nalo ni hili kwamba bishara hii, tangu mwezi Machi 1897 ambamo Lekhram aliuliwa, miaka 17 kabla ilielezwa kwa uwazi kabisa ndani ya kitabu chetu cha Barahine

Ahmadiyya. Na Barahin ilichapwa katika zama zile ambapo Lekhram labda alikuwa na umri wa miaka 12 au 13 hivi. Hili ndilo jambo linalopaswa kutafakariwa sana, na hili ndilo jambo litakaloongeza maarifa, na itaonekana tofauti ya wazi kabisa kati ya kitendo cha Mwenyezi Mungu na kitendo cha binadamu, na utulivu na amani itapatikana moyoni. Na aghalabu kulieleza jambo hili katika sehemu hii kutakuwa na faida kwamba hadi sasa ndani ya kijitabu changu kingine kiitwacho *Siraje Munir*, kwa ajili ya kuthibitisha kutokuwa kwangu na lawama na ukweli wangu, nimetoa mlolongo mwingine kama ushahidi, nao ni huu kwamba zile bishara zote zilizokwisha timia kabla ya kufa kwa Lekhram nimezikusanya na kuziandika ndani ya kijitabu hicho kilichotajwa na nimeuonyesha mpangilio wake kwa njia nzuri kabisa. Baadhi ya Waaria pia ni mashahidi wa bishara hizo ambao kuhusiana nao bishara hizo zilitolewa. Hivyo, kwa rai yangu itakuwa bora kwamba wanaofikiria afadhali wakione *Siraje Munir* wakati wa kuandika rai yao, basi waniombe, nami nitawatumia kijitabu hicho. Na jambo hili pia linafaa kuelezwa kwamba kama vile Waaria walivyo na shaka zisizo na haki kuhusiana na bishara hii, ambazo sababu yake si nyingine isipokuwa kwamba adhama ya bishara imewashitua, vivyo hivyo wale masheikh pia wanaotupinga ambao hawana ufahamu wa kiroho walivyoshikwa na titizo hilo hilo.

Hivyo, kijitabu hiki kitawafaidisha pia sharti wakisome kwa makini sana. Na kijitabu hiki kinatumwa kwako kwa njia ya barua hii kwamba kwa kuzitafakari sababu zilizotolewa kwenye kijitabu uandike fatwa ile iliyotokana na matashi ya uadilifu wa moyoni mwako, ambayo ni wajibu kuiandika kutokana na sababu zilizoelezwa, yaani, je ile bishara iliyotolewa kuhusiana na kifo cha Lekhram imetimia kwa hakika au la? Na je ilikuwa ndiyo ya daraja la juu lisilo la kawaida au la, ambayo kwayo yaweza kusemwa kwa yakini kabisa kwamba hiyo siyo njama ya kibinadamu wala si jambo lililotokea kwa bahati bali ni kitendo mahsusi cha Mwenyezi Mungu ambacho chapaswa kusemwa kuwa ni utabiri wa kiufunuo. Na amani iwe juu ya yule afuataye mwongozo.

Mwandishi, Ghulam Ahmad wa Qadian
8 Dhul Hijja mwaka 1314 Hijriyya

---

Narudia kwamba yule asiyependa kuandika – katika jedwali iliyoambatanishwa – ushuhuda wa kusadikisha ishara kuhusu Lekhram, itamlazimu kurudisha kitabu hiki Istiftaa pamwe na barua hii.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [2]

# TOENI FATWA

Wanasemaje waheshimiwa wenye busara na wenye rai, kwamba hizi shuhuda za kiufunuo ambazo zimeandikwa hapa chini, je kuzitazama hizi kunaongoza kwenye natija ya kutuliza au la kuwa ule utabiri uliotolewa kuhusiana na kifo cha Lekhram ulitimia kweli au hapana? Ikiwa katika rai yao, kwa yakini na makini kamili yathibitika kwa uwazi sana kutokana na bishara zilizoandikwa hapa chini zilizo kama ushuhuda ulioandikwa, kwamba maandiko yale yako mbali kabisa na makisio na njama za binadamu na yasiyo ya kawaida, basi kwa ajili tu ya Mungu, kwa kuusaidia ukweli – jambo wanalowajibikiwa wajasiri, mashujaa na wacha Mungu – waandike ushuhuda wao chini ya madhumuni haya kwa nia ya kusadikisha. Mimi nina yakini kwamba Mwenyezi Mungu Atawapa ujira wa ushahidi huo wa kweli na

---

1 Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

2 Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

Atawapatia sehemu kamili katika mafanikio na hali njema ya kidunia na ya kidini. La sivyo, matokeo mabaya ya kuuficha ushahidi wa kweli hakuna budi kudhihirika pia sawa na kanuni ya Mungu. Lakini ikiwa kwa rai ya mtu fulani shuhuda za kiufunuo zilizoandikwa hapa chini hazitulizi moyo, bali kwa rai yake, hizo kwa hakika zilikuwa ni njama za kibinadamu, ambazo zilienezwa kwa kisingizio cha utabiri wa kiufunuo, ambazo matokeo yake yakawa kwamba kutokana na njama hizo madhubuti Lekhram akauawa huko Lahore mnamo tarehe 6 Machi 1897, basi yeye mtu huyo anayo hiari kuwa asitoe ushahidi wake kwenye karatasi hii, na aendelee kunihesabu miongoni mwa wauaji. Lakini ikiwa, kwa rai yake, shuhuda hizi za kiufunuo zastahili kupimwa tunazostahiki kufaidika nazo, hapo hatutaki kwa wakati huu huruma ya kidini, bali huruma ya kibinadamu, na hiyo nayo sawasawa na uadilifu kiasi sheria inachotupatia haki, basi twaomba haki hiyo kwa adabu kutoka kwa watu wenye rai kwa njia ya kuuliza fatwa. Sisi twataka nini toka kwa watu wenye busara katika kuomba fatwa hii? Ni hii tu kwamba ule mlolongo mkamilifu uliopangwa tunaoweka mbele yao kuhusiana na bishara za kifo cha Lekhram wauandikie rai yao, kwa kutafakari sana, kwa njia ya

fatwa na watoe ushahidi uliotokana na raghba ya dhamira yao safi kwamba je akili na uaminifu hauwajibishi kwamba mlolongo huu wa funuo zisizo za kawaida unasibishwe kwa Mwenyezi Mugnu? Na je, inaweza kuingia akilini mwa mtu mwenye busara kwamba matawi yote haya ya bishara, yaliyozidi nguvu za kibinadamu, ghafula yakaibuka kuusaidia uongo? Hivi sasa yalazimu kueleza kwamba Waarya, kwa ajili ya kuikadhibisha ishara hii, hawana chochote zaidi ya hii kwamba badala ya kuzitafakari kazi za ajabu za Mungu, wao wakachagua njia hii kwamba kutokana na dhana mbaya, wakaupa welekeo wa kuwa njama za kibinadamu daraja lile linalohusika na kazi za Mungu Mweza. Kwa sababu bishara hii ilitolewa tangu zaidi ya miaka minne na jambo hili lilikwishawafikia Mabaniani kwa njia ya hotuba zilizotolewa katika mikutano kadha na pia kutokana na maandiko kwamba imeandikwa ndani ya bishara kuwa maisha ya Lekhram yatafikia hatima kwa njia ya kutisha sana, na pia kwamba kifo chake kitatokea ndani ya siku za Idi, na kitatokea ndani ya miaka sita, na bishara kwa maneno yake yaliyo wazi kabisa ilikuwa ikiashiria kwenye tukio la kuuawa, kwa hiyo walifikiri haiwezekani bishara itokayo kwa Mwenyezi Mungu iwe ina alama na ishara za wazi kiasi hicho.

Lakini wakafikiria kuwa haiwezekani mtu ayatamke kwa kinywa chake mambo yote haya ya ghaibu kabla ya kutimia kwake na halafu awe ameyatekeleza hivyo hivyo. Kwa hiyo, wakaichukulia bishara hii ya kiufunuo kuwa ni mpango wa kibinadamu na kwa kusisitiza mara kwa mara wakachapisha ndani ya magazeti kwamba kutoa bishara kwa uwazi namna hii na kubainisha tarehe na siku na sura ya mauti kabla ya kutokea, kwa njia ya wazi na isiyo na shaka, siyo desturi ya Mungu, bali ukweli ni huu kwamba huyu huyu mtu, yaani mwandishi wa kitabu hiki, ndiye muuaji wa Lekhram na bishara hiyo ni matokeo ya njama kubwa kabisa zilizofikiriwa na kupangwa kwa muda mrefu. Kwa msingi huu huu kwa kuafikiana wakatia shinikizo la kunifanya mimi kuwa mwenye kosa na katika kudhihirisha fikara yao hii wakaandika makala nyingi ndani ya magazeti na wakapeleka kisirisiri taarifa kwenye serikali hata kwamba mnamo tarehe 8 Aprili 1897 siku ya Alhamisi, maafisa wa Kiingereza walikuja Qadian na kuisachi nyumba yangu. Wakati wa upekuzi zikakutwa barua zenye saini ya Lekhram na pia yakakutwa yale mapatano ambamo yalikuwa yameandikwa masharti kuhusiana na kuonyesha ishara za kimbingu, na kwa ridhaa ya pande zote mbili, bishara ya kweli ilikuwa imefanywa

kuwa ndio kigezo cha kupimia ukweli na uongo. Basi, hayo yakasomwa mbele ya Mkuu wa polisi wa Wilaya ambayo madhumuni yake yalikuwa haya kwamba bishara ile itakayotolewa juu ya Lekhram itatoa uamuzi halisi kwa dini ya Islam na ya dini ya Waaria. Kama bishara itatokea kuwa ya kweli, basi itashuhudia ukweli wa dini ya Islam na itakuwa ni dalili ya ubatili wa dini ya Kibaniani. Na kama itatokea kuwa ni ya uongo, basi itashuhudia ukweli wa dini ya Kibaniani na – Mungu Apishe mbali – itatoa dalili ya ubatili wa dini ya Islam, na sharti hili Lekhram akaliandikisha kwa msisitizo wake. Na kwa kuwa mimi nilikuwa na yakini juu ya ahadi za Mwenyezi Mungu, kwa hiyo mimi pia nikalikubali. Sasa tatizo ambalo kwalo kumetokea haja ya kuomba fatwa hii si tu kwamba Waaria wametoa shutuma dhidi yangu ya kula njama za siri, bali baadhi ya wazee wa kaumu yetu pia wameafikiana nao na kutaka bishara adhimu kama hii, ambayo matokeo ya kuikadhibisha kulingana na karatasi za mapatano, ni kuikadhibisha Islam, kwa njia yoyote ionekane kuwa ni batili. Hivyo, Sheikh Abu Said Muhammad Husain wa Batala, mhariri wa gazeti la Ishaatus Sunnah na kadhalika baadhi ya masheikh wachache wameshachapisha kwa jumla rai hii kwamba bishara

hii ilithibitika kuwa ya uongo. Hivyo, alinitumia barua pia ambamo aliandika kwamba, “Mimi kwa nia yangu njema nimefikia uamuzi huu kwamba bishara haikutimia, yaani kifo cha Lekhram kilikuwa ni jambo la bahati tu ambamo hamna mkono wa Mungu hata kidogo”. Na akasisitiza kwamba kwa nini jambo hili likubaliwe kuwa imethibika kuwa bishara ilitokea kuwa ya kweli? Na kwa nini isikubaliwe kwamba haya yalikuwa ni mauti tu yaliyotokea kwa bahati ndani ya muhula wa bishara?

Hatungejali katu ukadhibishaji huu kwa ajili ya makusudio yetu binafsi, lakini kwa kuwa karatasi za mapatano zilikamatwa wakati wa upekuzi na zikasomwa mbele ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya, na kila adui na rafiki akapata habari yake, hivyo ukweli kama huu ambao kwa kuupuuza inashambuliwa Islam bila sababu, haustahili kutoangaliwa. Ni kutokana na haja hii iliyo muhimu kabisa, taarifa yote hii ilibidi ipelekwe kwa watu wenye busara ili waone kwamba ni dhuluma kubwa namna gani iliyokusudiwa. Inasikitisha kwamba watu hao wakati wa kudhihirisha mawazo hayo hawakufikiria kwamba kwa fafanuzi hizo hakuna bishara ya nabii yeyote yule itakayostawi duniani kwa sababu mlango wa wazo la kubuni upo wazi kila sehemu kwamba hilo limetukia

kwa bahati tu. Hivyo, kama rai hii ndiyo ya kweli, basi wanapaswa kukiri kuwa hakuna ithibati yoyote ya unabii wa manabii wote, na hayo yote yametukia kwa bahati tu.

Taurati na Kurani zimeichukulia bishara kuwa uthibitisho mkubwa wa unabii. Na mfasidi anaweza kuisema kwa urahisi bishara yoyote ya kweli kuwa ni jambo lililotukia kwa bahati tu. Lakini mimi ninasema kwa nguvu kwamba shuku zote hizi ni za aina hii kwamba kama vile Dahriya (mtu asiyeamini kuwepo kwa Mungu) kwa kusema uumbaji kuwa ni mlolongo ovyo anajizalishia mashaka juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na kuisema nidhamu nzima ya dunia kuwa ni jambo tu lililotokea kwa bahati. Na halafu anapokuja kufahamu na fadhili za Mungu zamfikia na anaushuhudia utaratibu kamili na madhubuti wa ulimwengu huu na anapata habari ya kiini cha uumbaji wa Mwumbaji na hekima zake za ndani basi huwa hana budi kulazimika kuachana na rai yake ya kwanza. Hivyo, yapasa kufahamu kwa yakini kwamba shutuma hizi pia ni za aina hiyo hiyo, na shutuma hizi huibuka moyoni wakati ule tu ambapo jiha zilizofichikana za bishara hazitazamwi na mpango wa kiungu wa Mwenyezi Mungu unafikiriwa kuwa wenye kasoro. Hakika yenyewe ni kwamba

mashaka ya aina hii daima huzalika ndani ya mioyo ya wale ambao mioyo yao haina maarifa ya kweli ya Mungu. Wao wakishangazwa na kazi za Mungu huelekea kwenye kukataa na huyatafutia matukio sababu ambayo kwayo fikira zao finyu na za kijuujuu zimegota, na huendelea kuikazania hiyo hiyo tu. Sisi twawauliza kwamba kama Lekhram alikufa kwa kuuawa kwa bahati tu, basi iliwezekana pia kwamba kwa bahati mtu yeyote asingedhamiria kumuua, au kama angedhamiria asingefanikiwa katika dhamira yake, au kama kwa kiasi fulani angemshambulia, basi kulikuwa na uwezekano kwamba asingekufa. Sasa kuna sababu ipi kwamba matukio ya jiha zote zingine yaliyoweza kutukia kwa bahati hayakutokea, lakini hili likatokea kwa bahati ambalo lilikuwa na matatizo mengi pia kuliko jiha zingine? Je hilo Akalifanya Mwenyezi Mungu au mtu mwingine? Basi Yule Mungu Mjuzi na Asikiaye sana Ambaye pande zote mbili zilimwachia kesi hii uadilifu Wake, na kuhusiana nayo upande mmoja ulipasha pia habari kuwa (Mungu) Amenidhihirishia kwamba Mimi Nitafanya hivyo hivyo, kwa nini idhaniwe juu yake kuwa Hakutoa hukumu ya kiadilifu, na kwa nini ifahamike kwamba Amemuhami mzushi? Kama iaminike kwamba hii pia ni desturi ya Mungu kuwa

Anazitimiza pia bishara za mwongo ambazo bishara hizo anazisema ni uthibitisho wa ukweli wake, basi ndiyo kusema kana kwamba dhamira ya Mungu kwa makusudi ni kwamba kwa kuwafanya waongo na wakweli kuwa sawa Aiangamize na Aipindue kabisa silisili nzima ya ukweli. Ikiwa ni sahihi kuwa Mungu Humhami mkweli na Huzitimiza ahadi Zake sio uzushi, basi itamlazimu muadilifu kuikubali kanuni hii kwamba ile bishara itolewayo kwa jina la Mungu nayo itimie, basi hiyo imetoka kwa Mungu. Na kama kanuni hii isiaminiwe, basi vitabu vyote vya Mungu havitabakia na dalili na njia za kuwa na yakini juu ya ukweli wake zitafungwa. Kwa mwelekeo huo huo Mwenyezi Mungu Anaashiria na kusema:

وَإِنْ يَكُ صَادِقًا يُصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِي يَعِدُكُمْ ط[3]

Yaani alama ya mkweli ni hii kwamba baadhi ya bishara zake hutimia. Sharti ya 'baadhi' imewekwa kwa sababu ndani ya bishara za maonyo inajuzu kutoadhibu katika hali ya kujirudi na kutubia, hata kama kusiwe na sharti lolote. Basi, yawezekana baadhi ya bishara za adhabu ziahirishwe na zisitimie ndani ya muda wake ulioahidiwa, kama vile ilivyotokea kwa kaumu ya Yunus. Ilmuradi, ile bishara itolewayo kwa

[3] Al-Mu'min, 40:29

jina la Mungu inapotimia, kuitilia shaka na kuichukulia bahati nasibu, inakuwa kama kuishambulia nidhamu ya kidini ya Mwenyezi Mungu na inakuwa ni dhamira ya kuliangusha jengo lote la unabii.

Baada ya kuyaandika hadi hapa mambo haya ya utangulizi, sasa tunatoa shuhuda hizi za ufunuo kwa kufululiza ambazo ni muhimu kuzijua kabla ya kuitolea fatwa. Na maswali ya vipingamizi yaliyoweza kujitokeza juu ya shuhuda hizi tumeshayajibu tangu mwanzo katika maelezo yaliyotolewa hapo juu na huenda hata hapo baadaye pia yakaandikwa kiasi fulani. Sasa, sisi kwa kuyaandika hadi hapa mambo haya ya utangulizi, kwanza twaandika zile barua za Pandit Lekhram na muhtasari wa makubaliano pamoja na jibu langu, ambavyo vilidhihirika kabla ya bishara hiyo kwa njia ya kuandikiana barua. Navyo ni hivi:

BARUA TOKA KWA PANDIT LEKHRAM: "Kwa mwenye daraja lenye baraka, bwana Mirza, Salamu! Tangu nimekuja hapa (Qadian), tumeshaandikiana mara nyingi lakini hayakutokea matokeo yaliyotakikana. Sasa kwa kuwa sina budi kufanya uamuzi bora kwa nia ya kuihakiki haki, kwa hiyo ningekusumbua bwana kwamba leo mchana upange

muda wowote ule uje ndani ya Madrasa, au mwenyewe ukipanga sehemu yoyote ile mbali na nyumba yako unifahamishe ili niweze kuhudhuria pamoja na ndugu Kishan Singh na Hakim Diya Ram na Pandit Nihal Chand Ji ili kufanya uamuzi pamoja nawe kuhusiana na ishara za kimbingu, funuo na mjadala, waila ukumbuke vizuri kwamba kwa upande wangu nimeshatimiza hoja. Kuyakwepa mapambano ya kuutafuta ukweli ni mbali na sifa ya wenye akili. Mnyenyekevu, mtafuta haki, Lekhram. Tarehe 5 Desemba 1885."

BARUA YA PILI YA PANDIT LEKHRAM

"Mhisani wangu Bwana Mirza, Salamu. Ujumbe wako kwa muhtasari kutokana na ulimi wa ndugu Kishan Singh na kwa ufafanuzi kutokana na ulimi wa Maulawii Din Muhammad na Muhammad Umar umefika ukiwa ni majibu ya barua yangu, wenye madhumuni ya kwamba mjadala ufanywe juu ya masuala mawili matatu ya dini ya Aria na dini ya Islam na ziwekwe kanuni za mjadala zinazokubaliwa na pande zote mbili. Hivyo, kwa kujibu nakuomba kwamba kusudio langu la kuja Qadian toka Peshawar lilikuwa ndio hili tu na hadi sasa nimekaa hapa kwa tumaini hili hili kwamba kwa kusadikisha miujiza yako na maajabu yako na makarama yako na funuo

zako na ishara zako za kimbingu nizishuhudie, na kabla ya kufanya mjadala juu ya mafundisho mengine yoyote, jambo hili hili litatuliwe vyema kwenye kikao maalum cha watu wenye heshima. Na kama usipoweza kulithibitisha hilo na kulikwepa basi mimi sikatai kamwe kufanya mjadala mwingine pia. Hapa jambo hili pia lapaswa kukumbukwa kwamba kuketi nyumbani mwako na kutoa uthibitisho mbele ya wafuasi wako ni jambo lingine, na kuthibitika katika kikao cha wanazuoni na wataalamu ni kitu kingine. Tafadhali lete jibu lililo sahihi na usilete udhuru wowote na vijisababu ndani yake. Mnyenyekevu Lekhram, toka Aria Samaaj, Qadian. Ninakuomba tena na tena kwamba kama unayo hata athari kidogo za ukweli basi uzionyeshe, waila kwa ajili ya Mungu, epukana na hayo. Juu ya manabii ni kufikisha tu. Lekhram."

BARUA YA TATU YA PANDIT LEKHRAM

"Shikamoo Bwana Mirza. Mimi navichukia sana visa virefu virefu vya alfu-lela. Hivyo, sipendi kuirefusha barua kwa kuyarudia rudia maneno. Kwa muhtasari ninaomba kwamba masharti yale yale (yahusikanayo na kuziona ishara za Mungu) ambayo mimi niliyatayarisha na kuyatuma ambayo unayo nakala yake, pamoja na masharti yako yanapaswa kupelekwa

kwa waamuzi wanne, yatakayoamuliwa na waamuzi hao. Sisi wawili twapaswa kuyafuata. Ni kauli ya mtu fulani mwenye busara: Shika kitu kimoja, na kishike imara. Mimi naitekeleza hiyo, lakini yasikitisha kwamba wewe huonekani kukaa imara kwenye jambo lolote lile. Ewe ndugu, hii lazima itakuwa kwamba (wakati wa kudhihirika ukweli au uwongo wa ishara ya kimbingu) ikiwa sharti kwa ajili yangu ni la kuikubali dini ya Muhammad, basi kwa ajili yako pia ni lazima kuikubali dini ya Aria. La sivyo, badala yake ni kutoa rupia 300. Kama Mwenyezi Mungu Akiushindisha ukweli, basi nitazichukua hizo fedha, waila fedha zako zitakabidhiwa kwako na juhudi yangu itapotea bure, na mapato yako yataongezeka. (Methali ya Kiajemi): *Kula tende pia, na kupata thawabu vilevile.* Una faraja na utulivu kwa nini una wasiwasi?... Nawe wadai kuwa Mujiibud daawati...[4]

---

[4] Kwa matumizi ya neno hili la 'Mujiibud Daawati', 'ujuzi' wa lugha ya Kiarabu wa Lekhram unathibitika kwa uwazi kabisa. Hata yule mtoto aliyesoma tu kitabu cha kwanza cha sarufi ya Kiarabu anafahamu kwamba neno Mujibu latumika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, yaani Mwenye kukubali maombi. Hiki ni kinyambuo cha Faail (Atendaye) kilichotoka katika ngeli ya If'aal. Kwa hiyo, Lekhram alipaswa kusema hivi kwamba wewe wadai kuwa Mustajaabud Daawati. Sasa hebu tafakarini kwamba ni uwongo mkubwa namna gani wa Waaria kwamba Lekhram alikuwa anakijua Kiarabu pia. Hizi ni zile barua

Na kama ukipenda maneno matupu hivyo tu, basi ni raha moja kwa moja. Basi uendelee na mawazo ya kutamani usiyoweza kuyapata, na usijali mtu yeyote duniani. Unayo hiyari, mkono ni wako na ulimi ni wako. Tangu nije hapa zimeshapita siku ishirini na tano, natarajia kuondoka kesho au keshokutwa. Kama wataka kufanya mjadala ni sawa, na kama unataka kuyatuma masharti (Yaani makubaliano ya kuonyesha ishara) kwa waamuzi basi uamue, waila baadaye haitafaa kujigamba katika marafiki zako. Lakini itakuwa ni bora kwamba leo hii hii uje kwenye uwanja wa Madrasa, utoe uthibitisho wa Shetani, Uombezi na kupasuka kwa mwezi na pia umteue mwamuzi wa kusimamia mjadala. Kwa upande wangu umfahamu Bwana Mirza Imamud Din kuwa mwamuzi. Ikiwa huwezi kutosheka hata na hii, basi kwa ajili ya Mungu, ujiepushe na hayo.

Mnyenyekevu, Lekhram.
13 Desemba 1885.
BARUA YA NNE: Bwana Mirza, salamu.
Barua yako ya karatasi mbili imenifikia ambayo kwayo imedhihirika kwa uwazi kuwa ndani ya Kurani

---

zilizoandikwa kwa mkono wake mwenyewe ziandikwazo hapa. Ukweli ni huu tu kwamba mtu huyo alikuwa hajui lugha zote mbili, hakujua Kisanskriti wala Kiarabu, na hatuwezi kuzuia ulimi wa anayesema uongo. Mwandishi.

tukufu mmejaa tu visa vya akina Ibrahim, Musa, Isa, Muhammad[saw], Yusufu, Luti, Iskandar na Lukman, na mambo ya kipuuzi. Mimi ninakubali kufanya mjadala kwa masharti yaliyomo ndani ya barua ya jana, nawe kwa uwazi unaendelea kufanya ujanja na kuahirisha mambo na kuhoji bure. Bwana Mirza, inasikitisha, inasikitisha kwamba wewe hutaki shauri likatwe. Ni kweli msemo huu usemao: Udhuru usiofaa unathibitisha kosa. Isitoshe, wewe ni Masihi wa pili. Ulithibitishe dai lako, waila usipige kelele zisizo na maana. Lekhram, kutoka Aria Samaj, Qadian. Majira ya saa tatu asubuhi.

BARUA YA TANO: "Bwana Mirza, kuchimba mlima (mbele yake kuna neno lilioandikwa kwa haraka, lisilosomeka). Ni masikitiko kwamba unachukulia farasi wako kuwa farasi na farasi ya wengine kuwa nyumbu. Mimi nimejibu kiakili shutuma dhidi ya Veda, nawe umetoa majibu ya shutuma dhidi ya Kurani kutokana na maandiko, lakini yako mbali sana na akili. Kama wewe huna nafasi, mimi pia nina kazi nyingi. Haya, onyesha basi hata ishara ya kimbingu. Kama hutaki kufanya majadiliano, Muombe Mola wa Arshi aliye mbora wa wafanyao hila, ishara yoyote

kunihusu mimi ili shauri liamuliwe.[5] Lekhram."

---

[5] Sehemu hii wakati wa kuomba ishara, Lekhram alimwita Mwenyezi Mungu jina Mbora wa wafanyao hila. (*Khairul Makirina*). Na neno *Makir* hutumika kwa Mwenyezi Mungu ambapo Yeye humuangamiza au kumdhalilisha mkosefu kwa njia zilizofichika mno. Hivyo toka kinywani mwa Lekhram yametoka yenyewe yale maneno yanayothibitisha kwamba alikuwa akiomba ishara ya mauti yake, yaani ishara ambayo sababu zake zimefichika mno. Hivyo, ni kudra ya Mungu kwamba kifo chake kikatokea hivyo hivyo, na aliuawa kwa mkono wa muuaji ambaye kazi yake inamshangaza mno kila mtu kwamba aliwezaje kumshambulia mchana kweupe, na aliwezaje kujasiri kuinua mkono ndani ya nyumba iliyokaliwa na watu, na aliwezaje kuondoka kwa urahisi baada ya kumdunga kisu, na halafu iliwezekanaje ndani ya mtaa wa Mabaniani uliokaliwa, muuaji hakuweza kukamatwa juu ya kwamba warithi wa aliyeuawa walipiga kelele za mayowe. Hivyo, tunapoyatafakari kwa makini matukio hayo, mara akili inaelekea upande huu kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ile ile kazi iliyostahili kunasibishwa kwa Mbora wa wafanyao hila. Tumeshaandika kwamba kwa mtazamo wa Kurani Tukufu, Mwenyezi Mungu huitwa jina *Khairul Makiriin* (Mbora wa wafanyao hila) wakati ule Anapomkamata mhalifu anayestahili adhabu, kwa kutumia sababu zilizofichika, yaani Huziandaa kwa ajili yake sababu zile za adhabu yake ambazo mhalifu hujiandalia mwenyewe kwa makusudio mengine. Basi sababu zile zile ambazo mhalifu hujikusanyia kwa kujitafutia heri au umaarufu, hizo hizo zinakuwa sababu za dhila na maangamizo yake. Kanuni ya maumbile inatoa ushuhuda wa wazi kabisa kwamba kitendo hiki pia cha Mungu chapatikana duniani

Kwa kuzijibu barua hizo zote, ziliandikwa barua kinaganaga ambazo si lazima kuzinukulu sehemu hii. Lekhram alikuwa na mazoea ya kuzusha na kuongopa sana, ndiyo sababu mara kwa mara anaandika ndani ya baura zake kwamba eti hufanyi mjadala, hunionyeshi ishara yoyote na hutoi majibu ya maana, ilhali kwa ajili ya mjadala njia hii safi kabisa iliwekwa mbele yake kwamba afanye mjadala kwa kujidhibiti tu

---

kwamba Yeye, wakati mwingine, Huwaadhibu wale wasio na haya na wenye mioyo migumu, kwa mikono yao wenyewe. Basi, watu hao huwa wanajikusanyia wenyewe sababu za dhila na maangamizo yao. Na mambo hayo huwa yanafichwa machoni mwao hadi wakati ule Kudra ya Mwenyezi Mungu iteremkapo. Hivyo, kulingana na kitendo hiki kilichofichika jina la Mungu ni *Maakir*. Kuna maelfu ya mifano ya aina hiyo inayopatikana duniani. Kwa hiyo katika suala la Lekhram, *Makr* (hila) ya Mwenyezi Mungu ni hii kwamba kwanza Alimfanya atamke kwa kinywa chake mwenyewe kwamba naomba ishara toka kwa *Khairul Maakiriin* (mbora wa wafanyao hila) kwa ajili yangu. Hivyo, ndani ya ombi hili akawa ameiomba adhabu ambayo sababu zake zimefichika, na ikatokea hivyo hivyo. Kwani, yule mtu ambaye kwa kumwingiza katika dini ya Aria, yeye aliiteua siku ya Jumapili, na siku hiyo ya Jumapili ikachukuliwa kuwa siku ya mkusanyiko wa furaha wa Waaria kama vile iwavyo siku ya Idi ili kumwingiza mtu huyo katika dini ya Aria, basi sababu hizo hizo za furaha zikawa sababu za maombolezo kwa ajili yake na kwa kaumu yake, na Mwenyezi Mungu Akawafahamisha vyema Waarya wote jina lake la *Khairul Maakiriin*. – Mwandishi.

ndani ya Veda na ajadili sawa na kutumia aya zake, nami nijadili sawa na aya za Kurani Tukufu tu. Basi, kwa kuwa yeye alikuwa jahili tu na pia hakuwa na uwezo wa kuleta aya za Veda katika kila sehemu, kwa hiyo kwa ujanja akawa hayaandiki yale tunayomdai, bali kwa kejeli na dhihaka akawa mara kwa mara anaomba ishara ya kimbingu. Ilmuradi, hapa twainukuu barua yetu ya mwisho ambayo iliandikwa kujibu barua yake ya mwisho, nayo ni hii:

"Mheshimiwa bwana Pandit, niliisoma barua yako. Fahamu kwa yakini kabisa kwamba sisi hatuukatai mjadala wala kuonyesha ishara, lakini wewe huitafuti haki kwa nia safi. Unaongeza masharti yasiyofaa, ulimi wako haukomi kutoa lugha chafu. Waandika, "Ikiwa hutaki kufanya mjadala, basi omba ishara yoyote ya kimbingu dhidi yangu toka kwa Mola wa Arshi, *Khairul Maakiriin*." Haya ni maneno ya dhihaka na kejeli kiasi gani, kana kwamba wewe humuamini Yule Mungu Awezaye kuwatanabahisha wajasiri. Na kuashiria kwamba Mungu Yuko juu ya arshi na Anafanya hila, basi hii ni kutokana na kutofahamu kwako. Mpango wa ndani kwa ndani na uliofichika unaitwa *Makr* ambao si makosa kuunasibisha na Mungu, na neno *arsh* latumika kwa ajili ya taadhima ya Mungu, kwa sababu Yu juu kuliko wote walio juu, Naye ni Mwenye ujalali, sio kwamba Yeye Anahitaji kiti cha enzi kama vile mwanadamu

yeyote. Imo ndani ya Kurani yenyewe kwamba Yeye Amekihifadhi kila kitu. Naye ni Mhifadhi Asiyetegemea kitu chochote. Sasa wakati Kurani Tukufu yasema hivyo, kuipinga arsh inakuwa ni dhuluma kiasi gani. Wewe hufahamu kabisa Kiarabu, hata maana ya *makr* pia huielewi. Ndani ya maana ya *makr* hamna jambo lolote lisilojuzu ambalo haliwezi kunasibishwa na Mwenyezi Mungu. Vile vitendo vilivyojificha mno kwa ajili ya kuwaadhibu wakorofi vinaitwa *makr*. Tazama kamusi ndipo utoe lawama. Kama mimi kulingana na kauli yako sina elimu ya Veda, kuna dhara gani, kwa sababu mimi najadili kwa kuzishika kanuni zako unazozikubali. Lakini wewe watoka nje ya misingi ya Kiislamu, wafanya uzushi dhahiri. Ilipaswa, kwanza ungeniuliza namna ilivyoaminiwa kuwepo kwa Mungu kwenye *arsh*, halafu kama kungebakia bado nafasi ndipo ungetoa lawama. Kadhalika ungeuliza kwanza maana ya *makr,* ndipo ungetoa lawama. Na ishara ziko kwa Mungu. Yu Mwenye uwezo wa kukuonyesha. Na amani iwe juu ya yule aliyeufuata mwongozo.

Mnyenyekevu, Mirza Ghulam Ahmad.

Na mapatano yale ya kuonyesha ishara yaliyofanywa kimaandishi baina yangu na Lekhram kichwa chake ambacho Lekhram mwenyewe alikiandika kwa mkono wake ni hiki:

Ee Mungu, twainama mbele yako, kwani U Mungu wa kweli. Dhihirisha ukweli, futilia mbali uongo, ili mafundisho ya kweli ya Veda yajulikane duniani.[6]

Halafu baada ya hapo, muhtasari wa makubaliano haya marefu ndio huu kwamba ikiwa bishara yoyote ile aambiwayo Lekhram isitimie, basi hiyo itakuwa ni dalili ya ukweli wa dini ya Kiaria, na ule upande uliotoa bishara utalazimika kujiunga na dini ya Kiaria au kumpa Lekhram rupia mia tatu na sitini ambazo zitakuwa zimewekwa kwenye duka la bwana Sharampat, mkazi wa Qadian. Na kama aliyetoa bishara atatokea kuwa mkweli, basi hiyo itakuwa ni dalili ya ukweli wa Islam na Pandit Lekhram atawajibika kusilimu.[7]

Halafu baada ya hapo ikatolewa ile bishara ambayo kutokana nayo maisha ya Lekhram yakamalizika

---

[6] Sharti hili kwamba Lekhram asilimu lilikuwa ni sharti la wakati ule ambapo ilikuwa haijulikani kuwa bishara ile itakayotoka kwa Mwenyezi Mungu itakuwa na madhumuni gani. Mwandishi.

[7] Lekhram aliomba dua hii kwa ajili ya matokeo ya bishara kwamba ikiwa Islam ni ya kweli basi bishara yake itokee kuwa ya kweli, na kama dini ya Kibaniani ni ya kweli basi bishara atakayotoa ithibitike kuwa ni ya uongo. Sasa twawauliza wasomaji kwamba kama bishara hii kuhusu Lekhram ifahamike kuwa ni ya uongo basi ni upande upi utakaopata athari mbaya ya dua hii? – Mwandishi.

mnamo tarehe 6 Machi 1897. Lakini kabla ya kumdhihirishia Lekhram bishara hiyo, mara nyingine, kwa njia ya tangazo la tarehe 20 February 1886, alipewa taarifa kwamba ikiwa kuitangaza bishara hiyo kutamhuzunisha basi isitangazwe, lakini Lekhram, kwa mbwembwe nyingi na ujasiri, kama lilivyotajwa jambo hili ndani ya tangazo la tarehe 20 Februari 1893, akanitumia barua aliyoisaini mwenyewe, akiandika kwamba: "Mimi ninazielewa bishara zako kuwa ni upuuzi tu, chapisha chochote ukitakacho juu yangu, nimekuruhusu na sihofu chochote kile". Hata hivyo tulicheleweshа sana, na pia kukawa na sababu hii kwamba mimi nilikuwa bado sijafunuliwa na Mwenyezi Mungu muda wa kutimia kwa bishara na Lekhram alikuwa akisisitiza kwamba bishara itajwe kwa muda wa kutimia kwake. Hatimaye mnamo tarehe 20 Februari 1893 baada ya kufanya maombi ya nguvu sana na kwa unyenyekevu, nikafahamu kuwa kuanzia tarehe ya leo, yaani 20 Februari 1893, ndani ya miaka sita, Lekhram atateremshiwa adhabu kali ambayo matokeo yake yatakuwa ni kifo, na pamoja na hayo ukafunuliwa ufunuo huu wa Kiarabu:

عجُل جَسَدٌ له خوار۔له نصبٌ وَ عَذاب۔

Yaani huyu ni ndama asiye na uhai ambaye ndani yake mnatoka sauti isiyo na maana, basi kwa ajili yake kuna pigo la huzuni na adhabu. Na kwenye ukurasa

wa 2 na 3 wa kipeperushi hicho kuna ibara hii: Sasa mimi baada ya kuichapisha bishara hii ninawadhihirishia Waislamu wote na Waarya na Wakristo na watu wa madhehebu mengine kwamba ikiwa mtu huyu, hadi kufikia muda wa miaka sita kuanzia tarehe ya leo, yaani tarehe 20 Februari 1893, kama hatateremkiwa na adhabu ya aina ya pekee, siyo kama masumbufu ya kawaida, na iliyo ya kimuujiza (yaani siyo katika yale masumbufu na maradhi ambayo ni ya asili na ya kawaida kwa mwanadamu ambapo pengine mwanadamu hupata kupona na pengine hufa), na iwe na jalali ya Mungu ndani yake (yaani alama za adhabu ya Mungu zipatikane ndani yake), basi mfahamu kuwa mimi sitoki kwa Mwenyezi Mungu wala kauli yangu hii haitokani na ufunuo Wake, (yaani ukweli na uongo wangu unategemea bishara hii hii). Na kama mimi nitokee kuwa mwongo katika bishara hii, basi niko tayari kupokea kila aina ya adhabu na niko radhi kwamba nitiwe kamba shingoni na kunyongwa. 20 Februari 1893.

Hapa waadilifu wafikirie kwamba katika hali ya bishara hii kutokea kuwa uwongo nilikuwa tayari kupata dhila gani, na ukweli na uwongo wangu ulikuwa umeitegemea bishara hii kwa daraja gani. Halafu wale wat wanaoamini uwepo wa Mungu na kulifahamu jambo hili kwamba kila kitu kinatokea

sawa na dhamira Yake, na hukumu ya mwisho ya kila mzozo hufanyika kwa mkono Wake, wao wanawezaje kusema kwamba kesi kubwa kama hii, ambayo matokeo yake yalikuwa yakisubiriwa na kaumu mbili kubwa, yalitokea tu kwa bahati bila ya elimu na dhamira ya Mungu; kana kwamba kesi ile iliyopelekwa kwa Mungu iliwekwa kando bila kuamriwa na mwamuzi pasipo yeye kujua. Kama mawazo ya aina hii yanastahili kutegemewa, basi silsila ya unabii wote na nidhamu yote ya sheria itavurugika mara moja. Kwani jambo ambalo lilidhihiri kama ushuhuda wa kimbingu baada ya changamoto na dai la msisistizo sana la adui na likadhihiri wazi wazi kulingana na alama zilizotajwa, kama hilo lifahamike kuwa ni upuuzi na batili, basi nini tena maana ya dini na ya uwepo wa Mungu? Bali kweli zote za kimbingu mara moja zitapotea bure.

Halafu bishara nyingine ya ufunuo iliyotokea kuhusiana na Lekhram, imetajwa kwenye ukurasa wa 54 wa *Karaamaatus Swaadiqiin* na kwenye ukurasa wa mwisho wa jalada. Nayo ni hii:

الا انني في كُلّ حرب غالب    فكدني بما زَوّرتَ فالحق يغلبُ
وبشّرني ربّي و قال مبشّرا    ستعرف يوم العيد والعيد اقربُ

و منها ما وعدنی ربّی و استجاب دعائی فی رجل مفسد عدوّ اللہ و رسولہ المسمّی لیکھرام الفشاوری۔ واخبرنی ربّی انّہ من الھالکین۔ انہ کان یسب نبیّ اللہ و یتکلم فی شانہ بکلمات خبیثۃ فدعوت علیہ فبشرنی ربّی بموتہ فی ستّ سنۃ ان فی ذالک لاٰیۃ للطالبین۔

Tafsiri: Mimi hushinda katika kila vita, yaani katika kila mapambano mimi hupata ushindi. Kwa hiyo, (Ewe Muhammad Husain wa Batala)! Hila yoyote uifanyayo bila shaka ifanye tu, lakini hatimaye haki ndiyo itakayoshinda. Na Mungu Akinipa habari njema ya ishara akasema: Karibuni utaitambua siku ya Idi, yaani siku ile ya furaha ambamo ishara ile itadhihirika. Na alama ya ishara ile ni hii kwamba siku ile itakuwa karibu na Idi ya kawaida. Na Mungu Ameniahidi na Ameisikia dua yangu kuhusiana na mfisadi mmoja aliye adui wa Mungu na Mtume[saw], ambaye ndiye Lekhram wa Peshawar na Amenipa habari kwamba atakufa. Yeye alikuwa akimtukana Mtume wa Mungu[saw] na kutumia mdomo mchafu. Basi mimi niliomba dhidi yake, na Mungu Akaikubali dua yangu na kuniambia kwamba yeye atakufa ndani ya muda wa miaka sita, na humo zimo ishara kwa wale wazitafutao.

Na ufunuo huu عجل جسدله خوار. له نصب و عذاب tuliouongelea sasa hivi, yaani Lekhram ni ndama wa Samirii, naye atapata adhabu kama huyo ndama. Huu ni ufunuo uliojaa maana ambao katika njia ya kufananisha na

ndama ya Samirii, unabainisha siri za hali ya juu kabisa za ghaibu. Mojawapo ni hii kwamba ndama ya Saamrii ilikatwa vipande vipande mnamo siku ya Idi ya Wayahudi kama vile ithibitikavyo ndani ya Taurati, Kutoka 32:5, kwamba: "Haruni akatangaza akisema, Kesho ni Idi ya Mungu". Basi, hivyo ndivyo karibu na siku ya Idi ya Kiislamu, yaani mnamo tarehe 6 Machi 1897, Lekhram aliuawa. Na kwa kuwa ndani ya vitabu vya Mungu siku ya Idi ndiyo ilikuwa mahsusi kwa ajili ya kuangamiza ndama ya Samirii, nalo lilikuwa ni tukio la siku ya Idi ambapo ndama ya Samirii ilisagwa sagwa kwa amri ya Mungu, hivyo Mwenyezi Mungu kwa kumwita Lekhram jina Ndama wa Samirii Akalitumia neno ambalo likawa linaongoza kwenye jambo hili kwamba Lekhram pia atauawa mnamo siku za Idi. Na ingawa wajuzi wa siri za ndani sana za maneno ya Mwenyezi Mungu wangeweza kufahamu kwa kumwita jina Ndama wa Samirii na tena kutajwa adhabu hiyo kwabma lazima mauti ya Lekhram pia, kuhusiana na siku yake, yatashabihiana na siku ya kuangamia kwa ndama wa Samirii, lakini hata hivyo Mwenyezi Mungu ndani ya ufunuo Wake hakutosheka tu na kueleza kwa ufupi, bali Akasema kwa maneno ya wazi sana kwamba:

ستعرف یوم العید والعید اقرب

Yaani, siku ya tukio la kuuawa kwa Lekhram itakuwa katika siku ambayo siku ya Idi itakuwa imeungana nayo. Na bishara hii kwamba mauti ya Lekhram yatatokea karibu na siku ya Idi, ilikuwa ni habari tuliyoishaitangaza sana hata kwamba alipouawa tu Lekhram, Mabaniani wakaloloma kwamba mtu huyu toka mwanzo alikuwa akisema kwamba Lekhram atakufa mnamo siku za Idi kama vile ndani ya magazeti ya Kibaniani ya 'Samachar Panjab[8] na mengineyo yalivyoshinikiza sana katika jambo hili. Inaonekana, baadhi ya Mabaniani wakorofi waliposikia maelezo ya bishara hii toka kinywani mwangu, waliyakumbuka wakati huo kama ni jambo lisilowezekana, kwa ajili ya kuja kunikosoa wakati fulani. Yaani, wakadhani kwamba ishara za wazi wazi namna hii kamwe haziwezi kutimia, nasi tutamwaibisha baadaye. Lakini Lekhram alipouawa kweli mnamo siku ya pili ya Idi, basi wakataka

[8] Ndani ya nyongeza ya gazeti la Panjab Samachar la tarehe 10 Machi 1897 mmeandikwa kuhusiana nami kwamba: "Alikuwa akisema kwamba atamuua Pandit na katika muda fulani na siku fulani (yaani siku ya pili ya Idi), atakufa katika hali ya kuhuzunisha sana." Hivyo, jambo hili kwamba "atamuua" amelibuni mhariri mwenyewe, lakini mtajo wa siku na sura ya mauti ulikuwa ni utashi uliojulikana wa bishara yetu yenyewe ambao bila shaka ulielezwa mara nyingi sana. – Mwandishi

kuzifanya bishara hizo kwa jiha nyingine zisiwe zenye kuaminiwa. Ndiyo kusema kwamba siku ya Idi iliwekwa mapema kwa kufikiria baada ya kushauriana. Lakini, kama hii ilikuwa ni kweli, kwa nini Lekhram hakupewa ulinzi kamili mnamo siku za Idi ili njama ile isingeliweza kutekelezeka ambayo Waaria walikuwa wakiifahamu tangu miaka kadha. Itifaki hii ya ajabu ilitokea kwamba siku ile roho ya Lekhram ilipotoka, yaani siku ya Jumapili, siku hiyo Waaria walikuwa wameifanya iwe siku mahsusi ya Idi yao. Kwanza siku yenyewe ilikuwa ni siku ya Jumapili ambayo ni mojawapo kati ya siku za Idi za Mabaniani, pili kwa kumpokea katika Uaria yule muuaji ambaye alijisema Yu mwislamu mpya wakawa wameipanga siku hiyo kuwa sikukuu ambapo walikuwa wamedhamiria kumrudisha muuaji katika dini ya Kibaniani katika mkutano wa hadhara.

Ilmuradi, jina la ndama ambalo ufunuo wa Mungu ulimpatia Lekhram, lilikuwa na siri ya ndani sana ndani yake, na madokezo mengi ya ishara za ghaibu yalikuwa yamejaa ndani yake. Mojawapo ni hii hii kupata ghadhabu ya Mungu ndani ya siku za Idi kama ndama ya Samirii. Ya pili ni hii kwamba ndama ya Samirii ilikatwa vipande vipande kwa mkono wa

mwanadamu na halafu akachomwa moto na kisha akatumbukizwa ndani ya mto. Hivyo mambo yote haya matatu yakadhihirika kwa Lekhram pia. Ya tatu ni hii kwamba ndama ya Samirii iliabudiwa, na Mungu Akatuma maradhi ya kuambukiza juu ya watu hao, ambayo aghalabu ilikuwa tauni. Kama vile ilivyo ndani ya Taurati, mlango: 32, aya: 35 [9] kwamba kwa sababu ya kutengeneza kwao ndama... Mwenyezi Mungu Akawapelekea hao maradhi ya kuambukiza yahilikishayo, halikadhalika kusifiwa kwa Lekhram kulifikishwa hadi ya kuabudiwa, na Waislamu wakaudhiwa bila haki yoyote. Hawa watu walikuwa wakifahamu vizuri ndani ya mioyo yao kwamba hicho ni kitendo cha Mungu, sio njama ya yule aliyeitoa bishara hiyo. Hata hivyo, wakatoa malalamiko ya mara kwa mara na kuifanya serikali ipekue nyumba yangu na baada ya kutoa kelele nyingi zisizo na maana wakashabihiana na waabuduo ndama. Nani ajuaye nini kitakachotokea baadaye, lakini sisi twaamini kwamba ule mfanano Alioueleza Mungu huo ni

[9] Kutoka, 32:35 [katika Biblia ya Kiurdu neno 'marii' limeandikwa, maana yake tauni au ugonjwa wa kuambukiza unaoangamiza watu wengi. Lakini katika Biblia ya Kiswahili imeandikwa: Bwana akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama. – Mwenezi]

mfanano kamili. Halafu kuhusiana na Lekhram kuna bishara nyingine ya ufunuo iliyotajwa kwenye kurasa za kwanza na mwisho za jalada ya kitabu cha *Barakaatud-Duaa*, na bishara hii ilitolewa mnamo mwezi wa Aprili 1893, yaani miezi mitatu baada ya ile bishara ya kwanza. Muhtasari wa maelezo ya bishara hii ni kwamba Sayidi Ahmad Khan K.C.S.I. aliandika kijitabu fulani kupinga kukubalika kwa maombi na akakipa jina *Risala Ya Adduaa wal Istijaabat*. Kijitabu hiki kilikuwa kinyume kabisa na ukweli, na kwa hiyo katika kukijibu nikaandika kijitabu cha *Barakaatud-Duaa.* Wakati wa kuandika kijitabu hicho nikahitaji niweke mbele ya Bwana Sayidi mfano wowote wa kukubalika kwa maombi. Na kwa fadhili za Mungu, katika siku hizo hizo, maombi yangu, kuhusiana na Lekhram yakawa yameshakubaliwa, hivyo nikauandika mfano huu katika ukurasa wa mbele wa kitabu cha *Barakaatud-Duaa*. Wasomaji wa *Barakaatud-Duaa* watakapokifungua kijitabu hicho basi kwenye ukurasa wa kwanza tu wa ukurasa wa mbele ambao ni ukurasa wa ndani wataikuta imeandikwa hivi kwa karatasi ya rangi:

## MFANO WA DUA ILIYOKUBALIWA

Kwa sababu hii hii kijitabu hicho kikaitwa jina *Barakaatud-Duaa*, kwani ndani yake mfano wa baraka za maombi umeonyeshwa. Kwenye ukurasa huu kuna ibara hii kuhusiana na Lekhram kwamba: Mimi ninakubali kwamba ikiwa, kama vile wapinzani walivyofikiria, matokeao ya bishara (imhusuyo Lekhram) hatimaye yatokee hivi kwamba imetokea tu homa ya kawaida au yametokea tu maumivu ya kawaida au kipindupindu kitokee halafu hali ya asili ya afya irejee, basi hiyo haitahesabika kuwa ni bishara... Hivyo, kwa sura hii, bila shaka yoyote, nitastahili kupata adhabu ambayo nimeitaja. Lakini kama bishara hii ikitokea kwa namna ambavyo ndani yake alama za adhabu ya Mungu zionekane kwa dhahiri na uwazi kabisa, basi hapo mfahamu kuwa hiyo imetoka kwa Mwenyezi Mungu... Ikiwa bishara, kwa hakika, idhihirike ikiogofya sana mno, basi hiyo yenyewe huivuta mioyo, na haya mawazo yote na shutuma hizi zote ambazo huzalika mioyoni kabla ya wakati hutoweka kiasi hiki kwamba watu waadilifu walio na busara wanajirudi rai zao pamoja na kuona haya. Isitoshe, mimi pia nipo chini ya kanuni ya maumbile. Ikiwa kwa upande wangu, msingi wa bishara hii ni kiasi hiki tu kwamba mimi kwa namna

ya upuuzi tu nimefikiria akilini mwangu maradhi machache ya kubahatisha na kuitangaza bishara hii kwa kukisia, basi yule mtu ambaye bishara hii inamhusu, naye pia anaweza kufanya hivyo kwamba atoe bishara kuhusiana nami kwa msingi huo huo wa kubahatisha... Ikiwa hiyo imetoka kwa Mwenyezi Mungu nami nafahamu vema kwamba imetoka kwa Mwenyezi Mungu, basi ni lazima itatokea pamoja na ishara yenye kutisha na itaitikisa mioyo. Na kama haikutoka Kwake, basi kudhalilika kwangu kutadhihirika. Na ikiwa mimi wakati huo nitatoa ufafanuzi mbovu, basi hiyo itakuwa ni sababu ya kudhalilika zaidi. Yule Dhati Aliye wa tangu azali na Mtakatifu na Mtukufu Ambaye hiyari zote zi mkononi Mwake huwa kamwe Hampi heshima aliye mwongo.[10] Hii si sahihi kabisa kwamba mimi nina uadui wowote binafsi na Lekhram. Mimi sina uadui binafsi na yeyote yule, bali mtu huyu alifanya uadui dhidi ya ukweli na akamtaja kwa kashfa yule

[10] Nilishasema wazi wazi hapo awali kwamba kwa kuwa Mwenyezi Mungu Hampi heshima mwongo, kwa hiyo kama mimi ni mwongo basi bishara hii kamwe haiwezi kutimia. Na pia nilisema kwa uwazi kabisa kwamba bishara hii ni kwa ajili ya kuidhihirisha heshima ya Mtume Mtukufu[saw]. Hivyo, yule asemaye kuwa bishara hiyo haikutimia, huyo anapaswa kukiri kwamba hapa Mwenyezi Mungu Hakuijali hata kidogo heshima ya Mtumesaw. – Mwandishi.

mkamilifu na mtakatifu aliyekuwa chemchemi ya kweli zote. Kwa hiyo Mungu Akataka kuidhihirisha duniani heshima ya mpendwa Wake. Basi.

Haya ndio yale madhumuni ya kuitilia nguvu bishara ile ya ufunuo iliyoandikwa kwenye ukurasa wa mbele wa *Barakaatud-Duaa*. Halafu kwenye rejeo, chini ya ukurasa huu huu, kuna bishara nyingine ya ufunuo kuhusiana na Lekhram ambayo kichwa chake ni hii: Habari nyingine kuhusiana na Lekhram wa Peshawar. Na mbele kuna ibara hii: "Leo tarehe 2 April 1893, sambamba na tarehe 14 Ramadhan 1310 Hijriyya, wakati wa asubuhi katika hali baina ya kulala na kuamka nilijiona kuwa nimekaa ndani ya jengo fulani kubwa, na baadhi ya marafiki zangu wachache pia wapo pamoja nami, mara mtu mmoja mwenye umbile lenye nguvu sana na sura ya kutisha, kana kwamba ameshikwa na hasira kali sana, akaja na kusimama mbele yangu. Mimi nikainua macho na kumtazama, nikafahamu kuwa yu mtu wa umbo na asili tofauti, kana kwamba si mwanadamu, bali ni miongoni mwa Malaika wakali wenye nguvu, na hofu yake ilienea nyoyoni. Nami nilipokuwa nikimtazama akaniuliza, 'Lekhram yuko wapi?' na akalitaja jina la mtu mwingine kwamba 'yuko wapi?' Ndipo wakati huo nikafahamu kuwa mtu huyo ametumwa kwa ajili ya kuwaadhibu Lekhram na mtu yule mwingine. Mimi

sasa sifahamu kuwa huyo mtu mwingine ni nani. Naam, hii kwa yakini kabisa nilikumbuka (yaani ndani ya hali ya kashfi ilipita moyoni mwangu) kwamba yule mtu mwingine alikuwa miongoni mwa wale watu wachache ambao nilishatoa matangazo juu yao, (yaani mtu yule ambaye alishalengwa na tangazo la bishara ya kifo ambaye kuhusiana naye inaweza kusemwa wakati wowote kuwa tangazo limeshatokea), na hiyo ilikuwa ni siku ya Jumapili na wakati wa saa kumi ya Alfajiri. Basi, kwa hiyo, sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. Basi.

Bishara zote hizo zinasema kwa sauti ya juu kuwa maisha ya Lekhram yalikuwa yamekadiriwa kumalizika kwa njia ya kuuawa, na ndiyo sababu lile shairi lililoandikwa mwanzoni mwa ufunuo unaohusiana na Lekhram humo mna maneno yanayoashiria kwenye kuuawa kwa Lekhram. Kwa hiyo tangazo lile la ufunuo lihusikanalo na mauti ya Lekhram ambalo limejumuishwa na kitabu cha *Aina Kamalate Islam,* beti chache za mwanzoni mwake zinazotoa dalili ya kuuawa kwake zaandikwa hapa chini, nazo ni hizi:[11]

[11] Hii ndiyo tafsiri ya beti za Kiajemi — Mwenezi.

Kuna nuru ya ajabu katika dhati ya Muhammad[saw], kuna kito cha ajabu katika madini ya Muhammad[saw].

Moyo unatakaswa na giza unapoingia katika marafiki zake Muhammad[saw].

Nashangaa kwa mioyo ya wajinga hao ambao wanakimbia meza ya chakula cha Muhammad[saw].

Simjui mtu yeyote hapa duniani wala akhera aliye na shani na heshima kama ya Muhammad[saw].

Mungu Anamchukia sana mtu aliye miongoni mwa wanaomchukia Muhammad[saw].

Mungu Mwenyewe Anamchoma moto Yule mdudu dhalili aliye miongoni mwa maadui zake Muhammad[saw].

Kama ukitaka kusalimika na upotevu wa nafsi, basi ujiunge na wapenzi wa Muhammad[saw].

Kama ukitaka kusifiwa na Mungu, basi uwe unamsifu Muhammad[saw] kwa moyo.

Kama unataka dalili ya ukweli wake, basi uwe mpenzi wake, kwani Muhammad[saw] mwenyewe ndiye dalili ya Muhammad[saw].

Rasi yangu yajitolea kwa vumbi la miguu ya Ahmad[saw], na moyo wangu wakati wote wajitolea kwa Muhammad[saw].

Naapa kwa shungi la Mtume wa Mungu kwamba najitolea kwa uso ung'aao wa Muhammad[saw].

Hata nikiuawa katika njia hii au nikiunguzwa, sitalipa kisogo jumba la Muhammad[saw].

Kuhusu dini siogopi hata ulimwengu wote, kwani ninayo imani kama ile ya Muhammad[saw].

kujitenga na dunia ni rahisi sana kwa kuzingatia uzuri na hisani ya Muhammad[saw].

Katika njia yake kila chembe yangu yajitolea, kwani nimeshajionea uzuri uliofichika wa Muhammad[saw].

Simjui mwalimu mwingine yeyote jina lake, kwani nimesoma katika madarasa ya Muhammad[saw].

Simjali mpendwa yeyote mwingine, kwani nimekwisha windwa na shani ya Muhammad[saw].

Miye nahitaji tu mtazamo wake, sitambui kitu pasipo bustani ya Muhammad[saw].

Msitafute moyo wangu uliojeruhiwa kifuani mwangu, kwani nimeisha utolea kwa dhati ya Muhammad[saw].

Miye ni ndege bora miongoni mwa ndege watakatifu ninayejikalia bustanini mwa Muhammad[saw].

Kwa penzi umenurisha roho yetu, uhai wangu ujitolee kwako, Ee Muhammad[saw].

Katika njia hii hata nikijitolea mara mia, bado nachelea hiyo hailingani na shani ya Muhammad[saw].

Nguli huyo amejaliwa kicho hata kwamba hakuna yeyote aingiaye uwanjani kukabiliana na Muhammad[saw].

Ee adui uliye mjinga na mpotofu! Ujihadhari na upanga mkali wa Muhammad[saw].[12]

Njia hii ya Mola iliyowapotea watu, uitafute katika ali na wasaidizi wa Muhammad[saw].

Jihadhari, Ewe uikanaye shani ya Muhammad na pia nuru dhahiri ya Muhammad[saw].

Ingawa karama imeshapotea kabisa, lakini njoo ukaione katika watumishi wa Muhammad[saw].

Utabiri moja kuhusu Lekhram wa Peshawar, hadi mwisho

(Kwa maelezo zaidi tazameni *Aina Kamalate Islam* uk. 1,2,3, rejeo chini ya ukurasa, mwishoni mwa kitabu)

Ilmuradi, mwanzoni mwa bishara hii kuna beti hizo cache ambazo katika hizo ubeti mmojawapo ni huu

[12] Ubeti huu ndio ufunuo wa Mungu.

pia:[13] بترس از تیغ بُرّان محمد ambao unaeleza kwa uwazi kabisa kwamba hatima ya Lekhram ilikuwa ni hii hii kwamba yeye auawe. Na kwenye ubeti wa mwisho mkono umechorwa ukiashiria kwenye 'Lekhram' kama ambavyo imeishachorwa sehemu hii, ili iwe ishara kwamba upanga mkali utamuangukia huyo huyo, na kutokana na kifo chake huyo karama itadhihirika.

Halafu kwenye ukurasa wa 28 wa *Barakaatud-Duaa*, ndani ya beti chache imedhihirishwa kwa Sayidi Ahmad Khan kwamba yeye asubiri tu ataona ndani ya bishara ya Lekhram mfano wa maombi yaliyokubaliwa. Na kwa kupiga mstari chini ya ubeti wa mwisho, Sayidi Ahmad Khan ameelekezwa kwenye kurasa za *Barakaatud-Duaa* ambamo umetajwa mfano wa maombi yaliyokubaliwa kwa kuyataja mauti ya kutisha ya Lekhram. Na beti zenyewe ndizo hizi:[14]

Uso wa Mpendwa haukufichikana kwa watafutao.
Huo ndio ung'aao katika jua na pia mwezini.

[13] Yaani uogope upanga mkali wa Muhammad[saw].

[14] Tafsiri ya shairi la Kiajemi.

Lakini uso huo mzuri umefichikana kwa walioghafilika. Mwenye kupenda anatakiwa kuwepo ili kwa ajili yake kifuniko cha uso kiondolewe.

Huwezi kumpata Mtakatifu Huyo kwa kiburi, kwa ajili yake hakuna njia isipokuwa unyenyekevu na kiherehere.

Njia ya kuelekea mtaa wa Mpenzi huyo Asiye na mwanzo ni ya hatari; ukitaka usalama na uhai wako, uachane na njia ya majivuno.

Fahamu na akili ya wasiostahiki haiwezi kufikia maana ya ndani ya Maneno Yake; kila atenganaye na majivuno, ndiye apataye njia iliyo sawa.

Mafumbo ya Kurani hayawezi kufumbuliwa na wana-dunia; yule tu aijua ladha ya mvinyo hiyo ainywaye.

Ewe usiye na habari yoyote ya nuru za batini, lolote utuambialo halitukasirishi.

Tumesema hayo kwa nasaha na huruma, ili jeraha hilo baya lipate kupona kwa marahamu hii.

Uyatibu maradhi ya kukana dua kwa dua, kama kitibiwavyo kileo kwa kileo wakati wa kulewa chakari.

Ewe usemaye kwamba kama dua zina athari basi hiyo athari iko wapi, nikimbilie haraka nikakuonyeshe hiyo athari kama jua.

Naam, usikatae siri hizi za kudra ya Mungu.

Katiza maneno, shuhudia kwetu dua ikubaliwayo.

Tazameni kurasa za 2,3,4, za jalada.

Hii sehemu ya pili ya ubeti wa mwisho ambayo baada ya kupiga mstari chini yake zimeandikwa 2,3,4, hizo zimeandikwa hivi hivi kwa kupiga mstari katika *Barakaatud-Duaa* ili Sayidi Ahmad Khan azitoe kurasa hizo na kuzisoma na ili kwa kuutafakari mfano wa dua yenye kukubaliwa apate uwezo wa kuachana na rai yake potofu baada ya kujaribu katika siku za usoni. Na kijitabu *Barakaatud-Duaa* kilipochapishwa, kilitumwa kwa Sayidi Ahmad Khan katika siku hizo bila kukawia, na hata jibu la Sayidi likaja pia kwamba ninakipitia *Barakaatud-Duaa.* Basi ni lazima kwamba Bwana Sayidi ameziona sehemu zile pia ambamo mfano wa dua yenye kukubaliwa umetolewa. Ilmuradi, ingawa kuomba dua kwa ajili ya kifo cha Lekhram kulisababishwa na midomo yake michafu na ujasiri wake, lakini hii pia ilikusudiwa kwamba mfano mmoja wa maombi yenye kukubalika utolewe kwa Bwana Sayidi. Sasa ni faradhi kwa Bwana Sayidi kuibadili rai yake hiyo mbovu, isiwe kwamba roho ya mtu mmoja imeondoka[15] na Bwana Sayidi

[15] Bishara moja kuhusiana na Lekhram ilikuwa يقضٰى امره فى ستّ yaani atafishwa ndani ya sita. Mpaka sasa sifahamu kama bishara

awe amebakia hapo hapo.

Hizi ndizo zile bishara ambazo zilichapishwa mno mnamo mwaka 1893 kuhusiana na kifo ya Lekhram, na mtu atakayezitafakari atalazimika kukubali kwamba ndani ya bishara hizo kwa hakika muhula wa miaka sita kuanzia tarehe 20 Februari 1893, ulielezwa kwa ajili ya kifo cha mtu anayetajwa hapa na kashfi pia ilikuwa ikidhihirisha kwamba kifo cha Lekhram kitakuwa mnamo siku ya Jumapili, kwa sababu yule malaika aliyekuja kwa kumwadhibu Lekhram alinidhihirikia mnamo usiku wa Jumapili, jambo ambalo lilimaanisha ya kuwa siku ya kifo cha Lekhram itakuwa ni siku ya Jumapili. Na hii pia

---

hii imepata kuchapishwa ndani ya tangazo letu lolote au kitabu au ndani ya maandiko ya rafiki yetu yeyote au la, lakini imeenea sana ndani ya Jumuiya yetu, na nina yakini kwamba bishara hii itakuwa imeshawafikia hata wengine kama vile bishara ya Idi ilivyowafikia Waarya, kwani habari yetu yoyote huwa haiwi ya siri. Bishara hii kama ilivyofahamika ilidhihirika hivyo hivyo, yaani Lekhram alijeruhiwa mnamo tarehe sita Machi na alijeruhiwa ndani ya saa ya sita ya mchana. Ikiwa Sheikh wa Batala anaikataa riwaya hii ya mdomo basi itamwia vigumu sana kuzikubali Hadithi, kwani hizo siyo tu ni masimulizi ya mdomo, bali ziliandikwa kwa uchache miaka mia hadi mia na hamsini baadaye. Jambo lililo la karibuni ambalo walioliona na kulisikia wapo hai, kulikataa hilo ni kudhalilika mbele ya wenye akili. Mwandishi.

ilidhihirishwa ndani ya ufunuo kwamba katika siku inayoambatana na Idi, yaani mnamo tarehe 2 ya Shawwaal, tukio hili litatokea. Na ni kudra ya Mungu kwamba habari hii ya Idi tangu mwanzo Mabaniani walikuwa wameikumbuka sana, lakini kwa wakati huo wakiliona jambo hili kuwa haliwezekani wakalikumbuka tu kwa lengo la kulikadhibisha. Kwani, kutokana na ujinga wao wakadhani kuwa haiwezekani katu kwamba ishara mahsusi ya aina hiyo iwepo ndani ya bishara nayo itokee kuwa kweli. Hivyo, katika kukumbuka, kusudio lilikuwa ni hili kwamba wakati bishara itakapokosea au isipotimia wakati wa Idi, basi hapo watacheka na kudhihaki. Lakini Mungu Alipoitimiza bishara kwa namna ile ile ilivyoandikwa, hapo mara moja Mabaniani wakageuka na kusema, "Mapema sana ilikuwa imeshafanyika njama ya kumuua mnamo siku ya Idi, waila hii siyo desturi ya Mungu kwamba Amuambie mtu mambo ya ghaibu kwa ishara mahsusi na yenye maelezo ya kina". Lakini Yule Mungu Mweza Asiyetaka kuutilia ukweli mashaka alikuwa anayapinga mawazo haya tangu mwanzo ambapo Mabaniani hawakuwa na habari nayo, yaani alitoa habari ya bishara hii ndani ya kitabu cha Barahine Ahmadiyya, miaka kumi na saba kabla ya tukio la kuuawa kwa Lekhram, na habari hii iliandikwa na

kuchapishwa wakati ambapo Lekhram alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili au kumi na mitatu, na hii imo ndani ya Baraahine Ahmadiyya kwa mpango na kwa kufululiza hata kwamba wanadamu hawana budi ila kuiamini. Sisi kwa fadhili za Allah tumeshaiandika ndani ya kijitabu *Siraje Munir,* nayo yamaanisha kwa muhtasari kwamba ndani ya funuo zilizomo katika Barahine Ahmadiyya imetolewa habari ya fitnia tatu dhidi yangu, yaani imeelezwa kwamba kwa nyakati tatu fitina tatu zitakukumba.

Sasa kabla ya kutaja fitina hizo tatu, ni muhimu kubainisha kwamba kila ukadhibishaji hauwezi kuitwa kuwa ni fitina. Bali katika hali hii tu ukadhibishaji utaitwa kuwa ni fitina wakati ukadhibishaji huo utakapokuwa kwa sura ya fujo, na kundi moja, kwa maafikiano, watumie nguvu zao kadri mtu awezavyo katika hali ya kichomo, kwa lengo la kumtia mtu fulani hasara ya mali, uhai au heshima. Hivyo, kwenye fitina ni lazima kundi fulani liwepo na kundi hilo kwa lengo la kumdhuru mtu fulani liafikiane kwa ari kubwa kabisa na katika hali ya vurugu wafanye mjumuiko wa hatari wakijiandaa kwa ajili ya kuishambulia heshima, uhai au mali ya mtu fulani, na kwa kushauriana wazitumie hila zote katika hali ya kushikwa na harara kwa jadhba isiyo ya kawaida ambapo kwa kuitumia kunakuwa na hatari

kwa ule upande mwingine kufikwa na balaa isiyotarajiwa. Sasa kwa kuwa ufafanuzi wa neno fitina umeshafahamika, basi ninazibainisha fitina hizo tatu. Lakini pengine kwa ajili ya kufahamisha, itafaa zaidi kwamba kabla ya kutoa maelezo ya fitina hizo tatu toka kwenye kurasa za Barahine Ahmadiyya, kwanza nizieleze fitina zile tatu ambazo zimeshanipitia baada ya kuandikwa na kuchapishwa kwa Barahine Ahmadiyya ambazo matukio yake yameshuhudiwa na malaki ya watu, na kama nikisema mamilioni, basi kwa hakika haitakuwa kutia chumvi. Wakati huu siwezi kukaa bila kukazania dai hili kwamba ile sehemu kubwa ya maisha yangu ambayo imetimia hadi sasa baada ya kuandika Barahine Ahmadiyya imepita chini ya fitina tatu sawasawa. Hakuna yeyote awezaye kuthibitisha kwamba kulikuwa na fitina nyingine yoyote pamoja na fitina hizo tatu inayopaswa kusemwa fitina ya nne, wala hakuna yeyote awezaye kudai kwamba hizo hazikuwa fitina tatu bali ni mbili. Ilmuradi, kwa idadi ya tatu imetiliwa mpaka kwamba idadi hiyo haiwezi kupungua wala kuongezeka. Hata mtu mgeni atakapoketi kuandika historia ya maisha yangu na kutafuta kuhusu maisha yangu kwamba kuanzia zama za Barahine Ahmadiyya hadi siku hizi, ghasia zisizo za kawaida zilizojaa jadhba kutoka makundi mbalimbali

ni kiasi gani zilizoishanififikia ambazo zinapaswa kuitwa fitina, basi katika kulifahamu jambo hili mtu huyo hatahitaji kufikiri kwamba fujo zile zilizofikia hadi ya kuwa fitina na kudhihirika kwa jadhba zote zilikuwa ni tatu tu. Kwanza ni shambulizi la Mapadre katika suala la Atham ambao wakiyaficha matukio wakavurumisha tufani la ukadhibishaji katika Panjab na India. Kwa kuwa mioyoni mwao kusudio kubwa lilikuwa ni kwamba kwa vyovyote wapate fursa ya kuikadhibisha na kuidhalilisha Islam.[16] Hivyo, wakati

[16] Ile bishara iliyotolewa kuhusiana na adhabu ya Atham ilikuwa bayana na kwa maneno waziwazi kabisa. Ndani yake mlikuwemo na sharti hili kwamba adhabu ya mauti itateremka ambapo Atham hatarejea kwenye haki. Na Atham kwa miezi kumi na mitano, ambayo ndiyo ilikuwa muhula wa bishara, aliachana kabisa na mijadala ya kidini na mihadhara kinyume na njia za mwenendo wake, na kukaa kimya kabisa, na kukaa kwake kimya kunatoa dalili ya kujirudi moyoni. Halafu baada ya kumalizika muhula huo alipotoa udhuru wa uongo kwamba 'mimi kweli nilihofu lakini hofu hiyo ilikuwa ni ya yule nyoka aliyepewa mafunzo maalum na ya mashambulizi mengine yaliyofanywa dhidi yangu.' Hapo alipoambiwa kwamba tuhuma zote hizo hazina uthibitisho na haziingii akilini na pia zimetolewa baada ya muhula ule kupita, anapaswa kuzithibitisha kwa kiapo au kwa njia ya kutoa malalamiko mahakamani au kwa njia yoyote nyingine ya binafsi, hakutumia njia yoyote, bali aliahidiwa kupewa rupia 4000 kama ataapa, hata hivyo hakuweza kudhihirisha kutokuwa kwake na hatia kwa kuapa na amezichukua lawama zote hizi ndani ya kaburi

wa uhai wa Atham walifahamu kuwa hakutakuwa tena na fursa nyingine yoyote bora zaidi ya kupiga makelele. Hivyo, kwanza kabisa huko Amritsar, kwa njia iliyo duni tu wakapiga kelele kwa kutaja yaliyo kinyume na yaliyotokea.[17] Na kwenye mitaa wakamchukua Atham na wakatumia midomo michafu ambayo mfano wake haupatikani wakati wowote tangu utawala wa Waingereza ulipokuja humu nchini. Na hawakutosheka na hapo bali wakafanya mikutano mikubwa mikubwa kuanzia Peshawar hadi Bombay, Kalkatta, Allahabaad n.k., na

---

lake. Ndani ya ufunuo wa Mungu kulikuwa pia na habari hii kwamba kama yeye ataueficha ushahidi, basi atakufa haraka. Hivyo, baada ya tangazo letu la mwisho yeye akafa ndani ya miezi saba. Sasa je kulikuwa na giza lolote juu ya bishara hii ambayo kwayo Wakristo waliipigia kelele? Hapana! Bali walikuwa na habari kamili juu ya Atham kuishi na hofu kiasi ya kwamba wakati fulani katika maradhi fulani Atham alipiga mayowe na kusema, "Hae, nimekamatwa". Lakini Wakristo waliridhia kuuficha ukweli. Katika kelele hizi walifanya dhuluma kubwa sana. Mwandishi.

[17] Mapadre walitumia sana njama hizi pia kwamba kwa hali yoyote Atham anishtaki ili niadhibiwe kupitia mahakama. Lakini kwa kuwa Atham kwa hakika alikuwa ameshakufa kwa hofu ya haki, kwa hiyo hakuelekea upande huu, bali akachapisha kwa uwazi kabisa ndani ya gazeti *Nur Afshan* kwamba vurugu hii ya Mapadre ilifanywa kinyume na ridhaa yangu. Mwandishi.

wakachapisha magazetini matukio kwa njia ya udanganyifu tu, na wakawachochea masheikh na watu wa kawaida na wakasambaza nchini maelfu ya vipeperushi vilivyojaa laana na wakataka kuwatilia watu athari hii kwamba dini ya Islam si chochote. Na baadhi ya Masheikh walio majibwa ya dunia wakashirikiana nao. Na fitina hii ilikuwa ni fitina kubwa kuliko zote, kwa sababu humo hakukuwa tu na mashambulizi juu ya dhati yangu, bali makusudio makubwa yalikuwa ni kwamba waionyeshe Islam kuwa ni dhalili na hakiri. Na Masheikh wenye sifa za Kiyahudi wakajumuika pamoja nao katika kukadhibisha na wakasema kwamba kama Wakristo wakadhibishe kuna dhara gani, huyu mtu mwenyewe ni kafiri, ilhali walielewa kwamba Wakristo wananielewa mimi pia kuwa Mwislamu, bali wananichukulia kiongozi wa kundi moja la Waislamu. Hivyo, hao wadhalimu, kwa sababu ya kuwa na uadui wangu pasipo haki wakaifanya dini ya Islam ichekwe kwa ndimi za Wakristo, bali mara kwa mara wakawashawishi wapeleke mashtaka dhidi yangu mahakamani.

Fitina ya pili, ambayo iko katika daraja la pili, ni fitina ya Sheikh Muhammad Husain wa Batala. Mdhalimu huyu pia alizusha fitina ambayo inakuwa vigumu kupata mfano wake ndani ya historia ya Islam katika

maisha ya wanazuoni waliopita. Akapigisha muhuri wa aliyepotewa na akili Nadhir Husain kusadikisha fatwa ya kukufurisha. Akawakufurisha mamia ya Waislamu na kuwasema ndio watu wa motoni, na kwa juhudi sana akachukuwa mashuhuda ya kwamba watu hawa katika ukafiri ni wabaya zaidi kuliko Wakristo. Mahusiano yote nao yamevunjika, ndugu wakatengana na ndugu, mababa wakatengana na wana wao, na wana wakatengana na baba zao, na ikaibuka tufani ya fitina sana kana kwamba limetokea tetemeko ambapo hadi leo maelfu ya waja wema wa Mungu na maulamaa na wanazuoni na wacha Mungu wa dini ya Islam wamefahamika kuwa makafiri na wanaostahiki jahanamu ya milele!!!

Fitina ya tatu iliyopo katika daraja la tatu ni fitina ya Waaria ambayo ilitokea pamoja na ishara ing'aayo. Na fitina hii ipo kwenye daraja la tatu kwa sababu ingawa ilikuwa na vurugu kubwa lakini pamoja nayo kulikuwa na ishara iliyo wazi ya ushindi. Hii ni kweli kwamba humo mlikuwa na kelele na fujo nyingi za Mabaniani, na mara kwa mara walitoa vitisho vya kuua na wakatuma barua zilizojaa matusi, ndani ya magazeti mengi maneno makali kupita kiasi yalitumika na mwishowe kwa njia ya serikali nyumba yangu ikapekuliwa, lakini juu ya mambo yote hayo bendera ya ushindi ilikuwa imebakia mikononi

mwetu. Yale mapatano yaliyofanywa pamoja na Lekhram ya kuipima dini kwa njia ya ishara ya kimbingu, kwa njia ya hayo Mola wetu Mkarimu Akitutolea hukumu dhidi ya Mabaniani akatupatia ushindi kwa uwazi kabisa. Na kama vile tangu mwanzo ndani ya Barahine Ahmadiyya kulikuwa na ufunuo huu kwamba kama Mungu Asingefanya hivi, yaani kama Asingeonyesha ishara yenye kung'aa namna hii basi machafuko yangepatikana duniani. Kadhalika Mungu Akatimiza dhamira zake zile zote. Lekhram kafa, na kawafisha Waaria wote; Islam ilipata heshima na Mabaniani wakadhalilika. Uwanja ukabakia mikononi mwetu kwa heshima kubwa na ikathibitika kwamba Mungu Ndiye Yule Yule Aliye Mungu wa Islam na Mwenye kuteremsha Kurani. Sasa kama kwa sababu hiyo, tulitukanwa, kama tulitishiwa kuuawa, kama nyumba yetu ikafanywa kupekuliwa, basi huzuni zote hizo si chochote mbele ya furaha hiyo. Bali kutokana na fitina hii, bishara nyingine imetimia ambayo tutaelezea sasa hivi na kwa kifo cha Lekhram adui alishadhalilika, lakini kusachiwa kwa nyumba yetu kumeziangamiza hila zao, na uwongo ukafutiliwa mbali vizuri sana.

Hizi ni fitina tatu zilizotufikia kuanzia zama za Barahin hadi sasa na hizo zimetokea kwa uwazi namna hii kwamba nina yakini kuwa kila mtu katika

nchi yetu mwenye haki ya kuitwa mwanadamu anazifahamu vizuri fitina hizo tatu. Sasa suala linalotakiwa kuamuliwa ni hili kwamba je fitina hizi tatu zimetajwa ndani ya Barahine Ahmadiyya au la? Basi, mimi naona kama mwanga wa mchana kwamba fitina hizo tatu kuanzia fitina ya mapadre hadi fitina ya ishara ing'aayo zimetajwa ndani ya Barahine Ahmadiyya, bali wakati kila mojawapo ilpotajwa neno fitina pia lipo hapo. Sasa, hebu, kwa moyo safi na mtazamo uliotakasika zisomeni ibara zifuatazo nilizozinukulu toka ndani ya Barahine Ahmadiyya na kuziandika hapa, nazo ni hizi:

Fitina ya kwanza, ukurasa 241 wa Barahine Ahmadiyya:

ولن ترضی عنک الیهود ولا النصاری. و خرقوا له بنین و بنات بغیر علم. قل هو اللّٰه احد اللّٰه الصمد لم یلد ولم یولد ولم یکن له کفوا احد. و یمکرون و یمکراللّٰه واللّٰه خیر الماکرین الفتنة هٰهنا فاصبر کما صبر اولوالعزم و قل ربّ ادخلنی مدخل صدق۔

Tafsiri: Yaani, Mayahudi hawataridhika nawe. Mradi wa Mayahudi sehemu hii ni wale masheikh wenye sifa za Kiyahudi ambao wametajwa kwenye ukurasa wa kabla ya huu wa Barahine Ahmadiyya. Na halafu Akasema Wakristo nao hawatakuwa radhi nawe, yaani mapadre. Na Akasema kwamba wao kwa ujinga wamefanya wana na mabinti wa Mungu. Waambie hao mapadre kuwa Mungu ni mmoja. Yeye ni Dhati

Asiyehitaji. Hana mwana wala Yeye si mwana wa yeyote yule, na hakuna anayefanana Naye. [Hii inaashiria kwenye ule mjadala uliohusiana na Utatu na Umoja wa Mungu uliofanyika kwenye nyumba ya Dr. Martin Clark huko Amritsar siku chache kabla ya kutolewa bishara]. Na halafu Akasema: Hawa Wakristo watakufanyia hila fulani na Mungu pia Atawafanyia hila, yaani kwanza Atawafanya kuwa wajasiri, halafu Atawapa dhila baada ya dhila. Na halafu Akasema: Mugnu ndiye Hufanya hila bora. Na kisha Akasema: Wakati huo kutakuwa na fitina toka kwa mapadre nao watakadhibisha kwa sura yenye fujo iliyojaa hamaki. Basi, ufanye subira wakati wa fitina hiyo kama vile walivyofanya subira manabii wenye imara na uombe dua kwamba Ee Mola, Udhihirishe ukweli wangu. Tulishaandika hapo awali kwamba *Makr* (Hila) mradi wake ni ule mpango latifu na uliojificha ambao hudhihiri toka kwa Mungu kumdhalilisha au kumuadhibu adui. Baadhi ya wakati adui aliye mjinga hupata utulivu kutokana na furaha fulani ya bandia, lakini mpango uliofichika wa Mungu, ambao kwa maneno mengine huitwa *Makr* (Hila), huwa unamwambia: Ewe mjinga, kwa nini wafurahi? Tazama siku zako za kudhalilika zimekaribia hapo zitaibadili furaha yako kuwa huzuni. Ilmuradi, hii ni fitina ya kwanza iliyoandikwa

kwenye ukurasa wa 241 wa Barahine Ahmadiyya na ambayo imeshanipitia.

Fitina ya pili ni ile iliyotajwa kwenye ukurasa wa 510 wa Barahine Ahmadiyya, nayo ni hii:

و اذ یمکر بک الذی کفر اوقد لی یا ھامان لعلی اطلع علٰی الٰہ موسٰی و انی لاظنّہ من الکاذبین. تبّت یدا ابی لھب و تب ما کان لہ ان یدخل فیھا الا خائفا. وما اصابک فمن اللّٰہ الفتنۃ ھٰھنا فاصبر کما صبر اولوالعزم. الا انھا فتنۃ من اللّٰہ لیحب حبّا جمّا. حبّا من اللّٰہ العزیز الاکرم عطاء ا غیر مجذوذ۔

Yaani, ikumbuke zama zile ambapo mkufurishaji fulani ambaye anaikataa imani yako atakufanyia hila na atasema: Ewe Hamani! Niwashie moto, [Yaani washa moto wa kukufurisha. Hamani mradi wake ni Nadhir Husain wa Delhi] mimi nataka kupata habari ya Mungu wa Musa kwa sababu mimi nadhani ya kwamba yeye ni mwongo. Abu Lahab ameangamia na mikono yake miwili imeangamia [Iliyoandika fatwa ya kukufurisha]. Hakustahili kujiingiza ndani ya kazi ya kukufurisha[18]. Na chochote kitakachokufikia, hicho kimetoka kwa Mungu. Sehemu hii kutatokea

---

[18] Firauni, mradi wake ni Muhammad Husain. Kashfi fulani toka kwa Mwenyezi Mungu inadhirisha kwamba yeye hatimaye ataamini, lakini sifahamu kama imani hiyo itakuwa kama ya Firauni ya kiasi hiki tu kwamba آمنت بالذی آمنت بہ بنو اسرائیل♦ au kama ya watu wema. Na Mungu ndiye Ajuaye zaidi. Mwandishi.

♦ Namwamini Yule wanayemwamini wana wa Israeli – Mfasiri

fitina fulani. Basi fanya subira kama vile manabii wenye imara walivyofanya subira. Kumbuka kwamba fitina hii itatoka kwa Mwenyezi Mungu ili Akufanye uwe rafiki wa kupita kiasi. Tazama, daraja lilioje hili kwamba Mungu amfanye mtu fulani kuwa rafiki. Yule Mungu ambaye jina Lake ni Aziz Akram [Mwenye nguvu Mkarimu sana]. Hiyo ndiyo ile neema ambayo kamwe haitokatishwa. Ndani ya fitina hii kuna neno wazi wazi la 'kaffara' ambalo kwalo inafahamika kwamba fitina hii itatoka kwa akufurishaye fulani; inajuzu pia kulisoma 'Kafara' limaanishalo 'mwenye kuikataa imani yetu'. Muradi wa maneno yote mawili ni mmoja tu. Ilmuradi, neno hili *kaffara* limetokana na *babu taf'il*,[19] na kwa kuangalia maana iliyotajwa linaweza kuwa *shina la kitenzi, yaani kafara, pia;* ufunuo upo katika sura zote mbili. Na sentensi ya baada ya hiyo, yaani: 'Hakupaswa kujiingiza ndani ya fitina hii ya kukufurisha', sentensi hii inaashiria kwenye jambo hili kwamba mtu huyo atakuwa na madai ya kuwa na elimu na ubora, yaani ataitwa kuwa ni Sheikh. Basi kwa sababu ya shani ile aliyokuwa akijidai kuwa nayo alitakiwa awe mbali sana kufanya kitendo cha kifasiki namna hiyo. Ilmuradi, hii ni fitina ya pili iliyo katika daraja la pili, iliyoandikwa kwa uwazi kabisa kwenye

[19] Mnyambuliko wa kitenzi taf'il katika Kiarabu – Mfasiri

ukurasa wa 510 wa Barahine Ahmadiyya.

Fitina ya tatu ni fitina yenye ishara ing'aayo ambayo imeandikwa dhahiri shahiri kwenye kurasa za 556 na 557 za Barahine, nayo ni hii:

يا عيسٰى انّى متوفيک و رافعک الىّ و جاعل الذين اتبعوک فوق الذين كفروا الٰى يوم القيامة. ثلّة من الاوّلين و ثلّة من الأخرين۔

Tafsiri: Yaani, Ewe Isa! Mimi nitakufisha kifo cha kawaida na Nitakunyanyua Kwangu na Nitawapa wafuasi wako ushindi juu ya wale watu wanaokukataa hadi siku ya Kiyama, na kundi moja la wafuasi litakuwepo kwanza na kundi lingine litakuwepo baadaye. Maneno haya ya kuliwaza ya Mungu yaliteremka kwa Hadhrat Isa[as] wakati alipokuwa katika hali ya mfadhaiko mkubwa na alikuwa ametishiwa mauti yaliyokuwa makhsusi kwa ajili ya watu wahalifu yaani tishio la msalaba yaliyo mauti ya laana. Na ufunuo huo huo na ahadi hiyo hiyo ilitolewa kwangu ambayo kwayo ilifahamika kwamba nitakumbwa na mtihani huu huu na hatima itakuwa ni hiyo hiyo. Kwa sababu hii hii nikapewa jina Isa, na nikaahidiwa kwamba: Mimi Nitakufisha kifo cha kawaida na Nitakunyanyua kwa heshima.

Ilmuradi, ndani ya ufunuo huu kuna bishara hii iliyojificha kwamba maadui zangu pia watafanya njama za kuniua kama ilivyokuwa kwa Hadhrat Isa[as],

na watafanya mipango ya kunifisha kifo cha wahalifu, yaani cha kunyongwa lakini hawatafanikiwa kutimiza dhamira hizo. Ilmuradi, kwa kuniita jina Isa ikaashiriwa kwenye sababu ya kupewa jina hili kwamba kwa namna ile ile kama ilivyoshauriwa na kupangwa kwamba kifo cha Hadhrat Isa[as] kiwe kile cha wahalifu hapa pia itatokea hivyo hivyo.

Halafu mbele ndani ya funuo zingine za baada yake imeashiriwa wazi kwamba hiyo itatokea lini na wakati gani, na dhamira za aina hii na mipango ya mauaji itakuwa katika zama zipi, na alama zipi zitadhihirika kabla ya hapo. Na ufunuo huo ni huu uliopo ndani ya ukurasa wa 557 wa Barahine Ahmadiyya:

میں اپنی چمکار دکھلاؤں گا اپنی قدرت نمائی سے تجھ کو اٹھاؤں گا۔ دنیا میں ایک
نذیر آیا پر دنیا نے اس کو قبول نہ کیا لیکن خدا اسے قبول کرے گا اور بڑے زور
آور حملوں سے اس کی سچائی ظاہر کردے گا۔ الفتنة ھٰھنا فاصبر کما صبر
اولوالعزم. فلمّا تجلّٰی ربّہ لِلجَبَل جعلہ دکّا

Ndani ya funuo hizi imeelezwa kwa uwazi kabisa kwamba mipango ya mauaji itakuwepo katika wakati ule ambapo ishara fulani ing'aayo itakadhihiri. Hii ndiyo sababu Akaziita njama hizo jina fitina katika ufunuo wa mwisho na Akasema kwamba hapa kutakuwa na fitina fulani, basi yafaa usubiri kama vile manabii wenye imara. Na pia Akasema kwamba mwishoni fitina hiyo itafutilika mbali.

Hizo ni fitina tatu ambazo zilitajwa ndani ya Barahin na zote hizo tatu pia zimetimia. Fitina kuhusu ishara ing'aayo haikuishia tu kwenye kelele na fujo za mdomoni, bali mnamo tarehe 8 April 1897 hata nyumba yangu ilisachiwa ili bishara ile itimie iliyokuwa imefichika katika kuitwa jina la Isa. Sasa kama vile kwa kuisoma Barahine Ahmadiyya yapatikana habari ya fitina hizo tatu, vivyo hivyo kama mtu asome historia ya maisha yangu ambayo hadi wakati huu yamekamilika tokea wakati wa Barahin, hapo pia atalazimika kuamini kwamba kwa nje pia fitina tatu tu zimetokea. Kutokana na utafiti huu sio tu ile bishara iliyotolewa kuhusiana na Lekhram inaimarika kwa thibitisho hizi zitiliazo nguvu, bali ile bishara iliyotolewa kumhusu Atham nayo pia yafunguka namna mchana unavyoangaza. Ilmuradi, kwa kuzitazama kwa makini fitina hizo tatu uwezo kamili wa Mungu unafahamika. Haya ni makamu ambayo hayastahili kuyaepa kwa kupayuka tu, bali yafaa kutafakari kwa makini sana. Bila shaka roho na dhamiri iliyotakasika ya mtafuta ukweli akipata habari ya makamu hayo yaweza kuokoka na mapazia mengi. Na bila shaka, kwa kawaida hapa swali linazuka kwamba ikiwa bishara zihusikanazo na Atham na Lekhram hazikutoka kwa Mwenyezi Mungu bali lilikuwa ni jambo la bahati tu, basi

zilipataje bishara zote hizi mbili kuandikwa ndani ya Barahine Ahmadiyya miaka kumi na saba iliyopita tangu sasa? Mtu mwadilifu anawezaje tena kulikimbia wapi jambo hili kwamba kama vile ambavyo kutokana na matukio yaliyotukia yapatikana ishara ya fitina tatu vivyo hivyo Barahine Ahmadiyya pia itoavyo habari ya fitina hizo tatu.

Sasa je shuhuda hizi zikiimarika kwa dalili nyingi hazijafikia kwenye daraja linaloitwa la yakini na lisilo na utata? Na je silsila hii ya ufunuo iendeleayo kwa miaka kumi na saba kutoka katika zama zetu hizi hadi zama zile zisizohusiana ambapo kalamu ya kutunga hila hukatika kabisa, haitoshi kwa ajili ya kupata utulivu kamili? Je hata sasa shaka yoyote imebakia ambayo mtu mwenye wasiwasi kitabia anaweza akaikazania? Na kusema kwamba Lekhram alikufa ndani ya mwaka wa tano na hakufa ndani ya mwaka wa sita, je kuna upumbavu zaidi ya kuleta shutuma hiyo? Huyu mtoa shutuma alisikia wapi na kwa nani kwamba ndani ya ufunuo mlikuwa na sharti kwamba lazima afe ndani ya mwaka wa sita? Ufunuo huo unaeleza kwa maneno ya wazi kabisa kwamba Mwenyezi Mungu Akificha wakati hasa wa mauti, Akatoa muda wa miaka sita kwa ishara kwamba ndani ya muda huo, wakati wowote Mungu Atakapotaka Lekhram atahilikishwa. Je, ni marufuku kwa Mungu

kulificha jambo fulani kwa hekima Yake na kulidhihirisha jambo lolote jingine? Shutuma za hovyo za namna hii zaweza tu kutoka kinywani mwa yule mpumbavu asiyekuwa na habari za falsafa za bishara za Mungu. Jambo lenyewe ni hili kwamba bishara zote zilizotimia duniani kupitia Manabii, humo ikakubalika kwamba kwa kiasi fulani nyakati za kudhihiri kwa bishara zifichwe pia. Hivyo, mara nyingi suna ya Mungu huwa kwamba kwa ajili ya kutokea kwa jambo fulani huwekwa kikomo fulani. Kisha huwa hiari ya Mungu, Akipenda Alitimize jambo hilo ndani ya sehemu ya mwanzoni ya muhula huo, na Akipenda Alitimize katika sehemu ya mwisho, na Akipenda Asiweke kikomo chochote wala Asieleze miadi yoyote. Ndani ya vitabu vya Mungu mtakuta mamia ya bishara ambazo wakati wa kudhihiri kwake haukutajwa. Hili ni jambo lililo wazi kabisa kwamba iwapo Mwenyezi Mungu Atoe ahadi fulani kwamba Nitalifanya jambo fulani hadi muda fulani katika wakati wowote Niutakao, je mwanadamu anaweza akatoa shutuma juu ya hili kwamba kwa nini hakuusema wakati makhsusi? Naam, kama Mwenyezi Mungu Akiweka miadi Aseme kwa maneno ya wazi kabisa kwamba maadamu miadi hii kamili haijapita na dakika yake ya mwisho au sekunde yake ya mwisho bado haijafika hadi hapo

bishara hii haitadhihirika, hapo katika sura hii italazimu bishara hiyo idhihirike katika sekunde ya mwisho ya miadi hiyo. Lakini kama Mungu kwa hekikma Yake Akadirie miadi na Adhihirishe kwamba ndani ya muhula huo, katika sehemu yoyote Nitakayoitaka, Nitalifanya jambo fulani, hapo kuilaumu bishara ya aina hii ndiyo sawasawa na kuyalaumu mambo yote ya Mwenyezi Mungu. Na ndani ya bishara imhusuyo Lekhram mna adhama hii kubwa kwamba humo hamkutajwa tu muhula wa miaka sita, bali hii pia ilisemwa kwamba yeye atapata adhabu yake ndani ya siku itakayoambatana na siku ya Idi.

Na ndiyo sababu Lekhram aliitwa jina ndama ya Samirii kwa sababu hii hii kwamba ndama ilichomwa moto mnamo siku ya Idi. Na ndani ya ufunuo wa wazi kabisa siku ya Idi ilitajwa na ilipata umaarufu kiasi hiki kwamba ufunuo huo ukajulikana kwa mamia ya Mabaniani. Na ilhamu na kashfi pia ilieleza hii pia kwa maneno ya uwazi kabisa kwamba mauti hayo yatakuwa ni ya kutisha na yatatokea kwa njia ya kuuawa, na kashfi pia iliashiria pia kwamba siku ya kifo itakuwa ni Jumapili na wakati utakuwa ni wa usiku.

Sasa tazameni, ni kwa namna gani zimejaa ndani ya bishara hii habari za ghaibu za hali ya juu. Sasa je hii si

sahihi kwamba ikiwa mambo yote haya yatazamwe kwa ujumla na kwa pamoja, na bishara ya Barahin pia iunganishwe nayo, bila shaka hutokea matokeo haya ya lazima kwamba bishara hizi sio za kawaida na ziko zaidi kabisa ya uwezo wa mwanadamu. Naam, kama kuna mwanadamu yeyote ambaye anayo nguvu ya kuweza kuzieleza ghaibu zilizojificha hivyo na kutoa habari za mambo hayo miaka kumi na saba kabla ambayo yalikuwa kama hayapo wakati wa kueleza kwayo, basi mtu wa aina hiyo anapaswa kutajwa kwa mfano, na matukio yake yanapaswa kudhihirishwa ili kuangaliwa, na visa tu vya zamani vilivyosahaulika havitafaa hapa.

نداریم اے یار با نَسِیَہ کار    اگر قدرتت ہست نقدے بیار[20]

Mmeshasikia kwamba ndani ya Barahine Ahmadiyya bishara zimeonyeshwa kwa uwazi kabisa, hivyo shuhuda hizi zifululizazo zitawezaje kuvunjika?

Kwa kuwa baadhi ya masheikh wadhalimu, kama vile Muhammad Husain wa Batala,[21] wanataka

[20] Ubeti wa Kiajemi: Ee rafiki, hatushughulikii kukopesha, lete fedha taslimu kama ukiweza.

[21] Sheikh huyu aliye adui wa haki pia amenizulia kwa kusema kwamba baadhi ya bishara nyingine pia zilitokea kuwa za uongo. Sisi tuseme nini zaidi ya haya kwamba Laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo. Sisi tuko tayari kutoa kwa kila bishara rupia mia moja, fedha taslimu, kwa Sheikh huyo

kuishambulia Islam kwa sababu tu ya kunifanyia uadui, na makusudio ya watu hao ni kuzifuta zile ishara zilizoteremka toka mbinguni kwa kutoa ushahidi wa ukweli wa dini hii, hivyo ombi hili la kutoa fatwa linapelekwa mbele ya waheshimiwa wenye busara wa kaumu. Tumeyaandika matukio yote na shuhuda zote sawasawa kabisa na vitabu ambavyo kutoka katika hivyo yameandikwa haya vimeshachapishwa tangu zamani. Kila mheshimiwa mwenye busara kama akitaka kuviona vitabu vyenyewe vya asili, basi anaweza kutuomba. Hivyo twawaomba waheshimiwa wenye busara kwamba wao, kwa ajili ya taadhima na heshima ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake[saw], waandike fatwa inayotokana na maelezo yaliyopo, kwenye kurasa zilizounganishwa na kijitabu hiki na kwa kuweka

---

aliyetajwa, kama aweze kuthibitisha kwamba bishara fulani ilitokea kinyume na ilivyotabiriwa. Lakini je akilisikia jambo hili atatuma maombi ya kufanya utafiti? Hapana, kwani kiburi kimempofusha. Nimefahamu kuwa mtu huyu ni mfisadi wa daraja la juu kabisa na ni adui wa haki. Ana uadui hasa na Uislamu. Moyo wake hautaki kwamba heshima, shani na utakatifu wa Islam udhihirike katika zama hizi zilizojaa vurugu, lakini yeye hatafanikiwa katika dhamira hii. Sikilizeni neno langu, likumbukeni vizuri tangu sasa kwamba Mwenyezi Mungu Ataonyesha ishara nyingi sana, Hatoacha hadi hapo atakapowadhalilisha watu wa aina hiyo. Mwandishi.

ushahidi wao na wa wengine, wawafanyie hisani watu waliopotea. Na watutumie maandiko hayo kwa njia ya barua, maana hayo yote kwa pamoja yatachapishwa. Nafahamu kwamba katika jambo hili shuhuda za watu wenye heshima na busara zitakuja kwa shauku toka kila upande na wale wakweli waaminifu kamwe hawataaficha ushahidi huo ambao kwao shani ya Islam hudhihirika, ila wale wenye asili duni, wenye mawazo duni na wenye kuiabudu dunia. Hivyo, watu wa aina hiyo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu Anasema kuwa yule atakayeuficha ushahidi wa kweli, moyo wake ni wenye dhambi kwa Mwenyezi Mungu. Kadiri ninavyoona, hata wale wenye vyeo serikalini hakuna kanuni yoyote inayowazuia kutoa ushuhuda wa kweli wa aina hii ambamo ukweli unasaidiwa kihalali. Ni sifa njema sana kwa mwanadamu kuuhami ukweli. Sisi hata kama tupate heshima na taadhima ya kidunia namna gani bado hatuwezi kwenda nje ya mkamato wa Mungu. Ni uzoefu wangu kwamba kutomtilia maanani huyu Hakimu Mwenye nguvu na kuficha ushahidi wa kweli ni kujinunulia pigo la kudhalilika. Yule mtu ambaye baada ya kuyaona maelezo ya wazi kabisa ya aina hii halafu ataepa kutoa ushahidi wa kweli, kuhusiana naye, itatubidi kwa uchache kumchukulia mtu huyo kuwa hajali kuihami heshima

ya Mwenyezi Mungu, dini na ya Mtume Mtukufu^saw^. Lakini kama atatoa ushahidi wa kweli, basi tutamuombea dua mbele ya Hakimu wa mahakimu kwa ajili ya kupata miradi yake ya kidini na ya kidunia. Nasi twaomba nini? Ni ushahidi tu wa kweli.

مبادا دل آں فرو مایہ شاد    کہ از بہر دنیا دہد دین باد[22]

Ninadhamiria kwamba mambo haya nikiyatafsirisha kwa Kiingereza niyapeleke pia kwa watu wenye busara wa Ulaya, kwani ndani mwao kwa asili mnapatikana ujasiri mkubwa wa kuuhami ukweli kwa sharti kwamba waufahamu ukweli kuwa ni ukweli hasa. Lakini kwanza ninapeleka maombi haya mbele ya ndugu zangu wa kaumu yangu na ninawapa fursa ya kutoa ushahidi huu wa kiume ambao kwa sababu yake majina yao yatadumu kuandikwa kwa heshima hadi mwisho wa dunia katika orodha ya watu wema.

Mwandishi,

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. 12 Mei, 1897.

[22] Isitokee hivi kwamba moyo wa huyu mdhalili ufarajike, anayeharibu dini kwa ajili ya dunia.

| Namba | Jina la msadikishaji wa Ishara imhusuyo Lekhram | Maskani pamoja na anuani | Maandishi ya kusadikisha |
|---|---|---|---|
| | | | |

| Namba | Jina la msadikishaji wa Ishara imhusuyo Lekhram | Maskani pamoja na anuani | Maandishi ya kusadikisha |
|---|---|---|---|
| | | | |